# Nipashe

Jumatano Mei 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580592

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**Mwinyi** ataja sababu Mwenge kutowekwa Makumbusho ya Taifa

UKURASA 4

**Polisi** adai kukuta magunia ya bangi gari lililopata ajali

UKURASA 4



**Ronaldo: Nimefikia malengo yangu Juventus**

UKURASA 21

# MTU KATI

• **Wabunge** waibana serikali kero nane Wizara ya Kilimo, limo sakata la korosho, kuporomoka bei za mazao... *Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), na Naibu Waziri, Hussein Bashe, wakifuatilia kwa makini michango ya wabunge katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WAFUGAJI KUTOLEWA HIFADHINI KWA OPERESHENI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk.Damas Ndumbaro, ametangaza operesheni ya kuwaondoa...

UKURASA WA 5



### TEMBO WAZIDI KUTIKISA, MBINU KUWAKABILI HIZI

WANANCHI wa vijiji vya Wilaya ya Namtumbo na Tunduru, mkoani Ruvuma wamepewa...

UKURASA WA 5

### MATATANI KWA KUSHINDWA KUELEZA FEDHA MAJI ZILIPO

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amelazimika kuwakabidhi mikononi mwa vyombo vya dola viongozi wawili wa jumuiya ya...




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Mfanyabiashara apigwa risasi dukani kwake

UKURASA 3



# TRA yatoa onyo risiti za bandia

UKURASA 2


**MICHEZO** MABILIONI YATOLEWA LIGI KUU BARA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Mhadhiri Mwandamizi wa Shule Kuu ya Sayansi na Teknolojia za Uvuvi, Paul Oyango (kushoto), kuhusu uzalishaji wa samaki aina ya kambale, wakati wa maonyesho ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wabunge waibana serikali

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wameibua hoja nane wakitaka serikali kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha kilimo nchini na kuwa na tija kwa wananchi wote hasa asilimia 65 wanaokitegemea.

Jana wakati mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2021/22, watunga sheria hao walisema bila hatua madhubuti, kinachojadiliwa ni siasa ambayo haiwezi kumkomboa mkulima.

**MASOKO, PEMBEJEO**

Mbunge wa Madaba, Joseph Mhagama (CCM), alisema soko la mazao ya wakulima ni mwarobaini wa mapinduzi ya kilimo, akisisitiza kuwa bei ya mazao ya wakulima wa Mkoa wa Ruvuma ni sawa na alichokiita dhuluma.

Deo Sanga, Mbunge wa Makambako (CCM), alisema mkoani Njombe na Iringa kuna mahindi mengi na hakuna soko na sasa debe linauzwa Sh. 3,000 hadi 4,000.

"Ili mkulima anunue mbolea ni lazima auze magunia mawili ili apate Sh. 110,000 ya mbolea. Ninaomba serikali imwangalie mkulima gharama za uzalishaji ni kubwa kuliko wanachokipata," alisema.

Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, alisema wakulima wanateseka kwa kukosa masoko ya bidhaa zao na kuna madalali wanaowakopa mazao tangu yakiwa shambani kwa bei ndogo.

Esther Maleko, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), alisema wakulima wanalima lakini hawajui watapata wapi masoko na kwamba imefika wakati wa kuwa na viwanda vya kuongeza thamani mazao badala ya kuuza ghafi.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Kenani (CHADEMA), aliuzungumzia umuhimu wa masoko, akitaka nchi iwekeze pia kwenye utafiti.

Alisema inashangaza kuwa asilimia 60 ya mbegu zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Mbunge wa Viti Maalum, Regina Ndege (CCM), alisema wakulima wengi wamekata tamaa kutokana na kukosekana kwa pembejo za kilimo.

"Masoko ni tatizo kubwa, wakulima wanauza mazao yao kwa bei ndogo sana, madalali wananunua mazao yakiwa shambani na mwisho mkulima ameendelea kuwa na maisha duni," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Judith Kapinga (CCM), alisema kwa miaka mitatu mfululizo wakulima wa mahindi mkoani Ruvuma hawana masoko huku wakidhulumiwa na madalali na kwamba Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) umeshindwa kuyanunua.

**MIUNDOMBINU**

Mbunge wa Madaba, Mhagama, alisema maeneo mengi nchini yana shida ya miundombinu kiasi cha wakulima kushindwa kuyafikia masoko.

Aliitahadharisha serikali dhidi ya mifumo ya kilimo cha mkataba, stakabadhi ghalani ambayo ina hasara na faida zake, akisisitiza sasa imekuwa sehemu ya kunyonya wakulima.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond, aliitaka serikali kusambaza mbegu mpya za alizeti nchi nzima ili kila mkulima azalishe na kushauri kuanzishwa kwa mafuta ya kupikia yatakayoitwa Samia.

**BENKI YA WAKULIMA**

Mbunge huyo alisema Benki ya Wakulima bado haijawafikia wakulima wadogo jambo linaloonekana benki hiyo ni kwa ajili ya wakubwa pekee kiasi cha kupoteza maana ya kumkomboa mkulima.

Hoja hiyo pia iliguswa na Sanga aliyesema ni muhimu benki hiyo kuwa na matawi wilayani ili kuhudumia wakulima kwa ukaribu zaidi, tofauti na sasa ambapo lazima mkulima asafiri hadi Dar es Salaam ili kupata huduma.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi, aliyesema benki hiyo inapaswa kuwa na matawi wilayani badala ya kuwa mjini.

**PARACHICHI**

Sanga alisema zao la parachichi ni kubwa nje ya nchi, lakini vifungashio vinavyotumika ni vya Kenya na linaposafirishwa kwenda nje huonekana linatoka nchi hiyo jirani.

Mbunge Raymond aliitaka serikali kusambaza mbegu za kisasa za parachichi mkoani Kilimanjaro ili wakulima walime ya kisasa na kupata faida kubwa.

**MAOFISA UGANI**

Mbunge wa Viti Maalum, Conjesta Rwamlaza (CHADEMA), alisema kuna uhaba mkubwa wa maofisa ugani kwa kuwa waliopo ni 6,700 huku mahitaji yakiwa 14,000 na wengi wako maeneo ya miji.

**USHIRIKA**

Mbunge huyo pia alihoji kazi ya ushirika nchini kwa kuwa kwenye maeneo mengi badala ya kusaidia mkulima, umegeuka kununua mazao ya wakulima.

Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei, alisema ni muhimu kupitiwa upya kwa Sheria ya Ushirika ili kuondoa viongozi wasiofaa na kubaki na wataoweza kuuinua.

Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa (CCM), alisema kama ushirika hautakuja na mbinu za kunufaisha wakulima, hakuna mapinduzi kwa kuwa sasa umekuwa mkopaji wa wakuma bila kuwalipa.

**STAKABADHI GHALANI**

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Kunti Majala, alisema Mkoa wa Dodoma hautaki stakabadhi ghalani kwa kuwa umekuwa mfumo kandamizi dhidi ya wakulima.

**UMWAGILIAJI**

Kunti pia alisema serikali bado haijatilia mkazo kuinua kilimo cha umwagiliaji badala yake bado inategema kilimo cha mvua, ambacho hakijawa na tija kwa miaka mingi.

Alitoa mfano kuwa bajeti ya umwagilijia ya Sh. bilioni 17 lakini fedha za ndani zilizotarajiwa kutolewa ni Sh. bilioni tatu, lakini hajjatolewa hata shilingi moja, zikiwa zimebaki siku 35 kufika ukomo wa mwaka wa fedha.

"Serikali haijatoa hata shilingi moja halafu unatarajia kuboresha kilimo cha umwagiliji! Imefikia mahali ninachoka kujadili bajeti ya kilimo kwa kuwa kila mwaka mambo ni yale yale, hatuoni mabadiliko," alisema.

## TRA yaonya risiti bandia

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imetoa onyo kwa wafanyabiashara wote wanaoendelea kufanya biashara zao bila kuzingatia utoaji wa risiti za kielektroniki (EFD) na wanaotoa risiti bandia.

Ofisa Elimu wa Huduma kwa Mlipa Kodi, Isihaka Sharifu (pichani chini), alitoa onyo hilo jijini Dar es Salaam jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni ya mamlaka hiyo ya utoaji wa elimu mlango kwa malango kwa wafanyabiashara walioko Kariakoo iliyoanza Mei 17, mwaka huu, kwa lengo la kutoa elimu kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kutoa risiti kwa wateja.

Alisema kitendo cha mfanyabiashara kuuza bidhaa bila kutoa risiti kinachochea ukwepaji kodi na kuikosesha serikali mapato na hivyo pato la taifa kupungua.

"Unapouza bidhaa bila kutoa risiti unakwamisha juhudi za serikali kukusanya kodi yake ipasavyo. Kwa hiyo, niwaombe wafanyabiashara kuwa wakweli na wenye uzalendo katika hili, lakini hata kwa mteja anatakiwa kudai risiti kwa kuwa ni haki yake ya msingi.

Aliongeza kuwa lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwasogeza wafanyabiashara karibu na kuendelea kutatua kero zinazowakwamisha kibiashara.

Ofisa huyo alikemea vikali wafanyabiashara wanaotoa risiti bandia, akifafanua kuwa utaratibu huo unakwenda sambamba na risiti ambazo hazilingani na bei ya bidhaa kwa lengo la kukwepa kodi ama sababu zao binafsi.

Alibainisha kuwa muuzaji akikamatwa kwa kosa hilo atapigwa faini ambayo ni kati ya Sh. milioni 1.5 hadi milioni 4.5 huku mnunuzi akipigwa faini kuanzia Sh. 30,000 hadi milioni 1.5.

Mfanyabiashara wa Kariakoo, Ramadhani Salum, alikiri elimu waliyopata imewabadilisha uelewa na kuwapa morali ya kazi.

"Kwa sasa uelewa umeongezeka, mwanzoni tulikuwa hatujui ukikosea kuandika pesa kwenye risiti ufanyaje lakini sasa hivi tunajua lakini hata mahali pa kupeleka malalamiko tulikuwa hatuna, sasa tumepajua.

"Tulikuwa hatujui umuhimu wa kutoa risiti lakini sasa tumejua. Kwa hiyo, elimu wanayoitoa ni nzuri na inatusaidia sana," alisifu.



HABARI KITAIFA

# Mfanyabiashara apigwa risasi

**Na Maulid Mmbaga**

MFANYABIASHARA wa duka la jumla lililoko Mabibo, Dar es Salaam, amenusurika kifo baada ya kujeruhiwa kwa kupigwa risasi na watu wanaodhaniwa majambazi ambao hawakufanikiwa kupora chochote.

Tukio hilo lilitokea juzi ikiwa ni siku ya nne tangu kuuawa kwa aliyekuwa Meneja wa Mauzo wa Kampuni ya Vodacom, Jimson Kibiti, mkazi wa Mbezi Beach, aliyepigwa risasi akitoka benki na kuporwa Sh. milioni nne.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Camilius Wambura (pichani), alibainisha hayo jana wakati wa kikao kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo.

Alidai mfanyabiashara huyo alipigwa risasi na watu wanaodhaniwa majambazi akiwa ndani ya duka lake lakini hawakufanikiwa kupora kitu chochote.

Kamanda Wambura alisema mfanyabiashara huyo anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wakati msako wa polisi ukiendelea dhidi ya wahusika.

Kamanda Wambura alitaja takwimu za matukio ya uhalifu yaliyotokea mkoani humo kwa muda wa siku tisa kuanzia Mei 8, mwaka huu, akibainisha kuwa wamekamata watuhumiwa 20 wakiwamo wanaodaiwa kupora silaha ya askari wa SUMA JKT na wengine wanaodaiwa kuvamia baa na kuua mlinzi.

Kamanda Wambura alisema Mei 18, mwaka huu usiku, watuhumiwa wa ujambazi walivamia nyumbani kwa Mkurugenzi wa Benki ya Azania, Mbweni Mpiji na kuwashambulia walinzi wa SUMA JKT na kuwapora silaha aina ya short gun pump action iliyokuwa na risasi tano.

Alisema kuwa siku mbili baadaye, Jeshi la Polisi liliwakamata watuhumiwa watano pamoja na silaha hiyo iliyoporwa.

Kamanda Wambura alisema Mei 8, mwaka huu, wahalifu walivamia baa ya Imbizo iliyoko Mikocheni A mkoani Dar es Salaam na kumpiga mlinzi, Regan Sylivester, kwa panga na rungu na kusababisha kifo chake.

Alisema katika tukio hilo wamewakamata watuhumiwa watano ambao ni: Issa Karim (33), maarufu Mdaka Bomu, mkazi wa Mbezi; Mohamed Juma (31), maarufu Mabangi, mkazi wa Mbezi Mwisho; na Selemani Seif (34), maarufu Dullah Kishandu, mkazi wa Mbezi Mwisho.



Wengine ni: Samson Joseph (32), maarufu Mjeuri, mkazi wa Mbezi; na Ezekiel Kennedy, maarufu Simba MC, mkazi wa Mbezi. Kamanda Wambura alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kuhusika katika tukio lingine la unyang'anyi wa kutumia silaha lililotokea Mwabepande Mei 7, mwaka huu, katika Kituo cha Mafuta cha MEXONS.

Alidai watuhumiwa hao waliwashambulia walinzi, watoa huduma na wateja na kupora Sh. milioni 2.4 na kuondoka na silaha ya mlinzi aina ya shot gun.

Katika tukio lingine, Kamanda Wambura alisema wanawashikilia watuhumiwa wanne ambao wanadaiwa kujihusisha na wizi wa magari na pikipiki maeneo ya Kinondoni na Ilala na miongoni mwao ni mtoto wa miaka 16.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni: Babuelly Chao (43), mkazi wa Moshi; Sebastiani Shembaru (36), mkazi wa Kigamboni; Hussen Misanya (33), mkazi wa Mabibo Relini; na mtoto huyo.

Alidai watuhumiwa hao walikutwa na magari manne ambapo mawili ni aina ya Toyota IST, Toyota Nadia na Toyota Mark II Grand na pikipiki moja aina ya boxer nyeusi iliyoibwa Mei 15, mwaka huu, eneo ya Kibamba Shule na kupelekwa Gairo mkoani Morogoro.

Vilevile, alisema wanawashikilia watu watano kwa tuhuma za kujihusisha na uvunjaji nyumba usiku na kuiba na wengine sita kwa uvunjani maduka katika maeneo ya Kariakoo na Ukonga Banana.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, katika mkutano huo, alitoa wito kwa wakurugenzi wa taasisi za fedha, zikiwamo benki, kutoa ushirikiano kwa vyombo vya usalama ili kukomesha vitendo vya uhalifu vinavyotokea katika mazingira yao.

"Niwaombe watu wa benki mtoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika usafirishaji wa fedha, mkae na watumishi wenu wa benki, watoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi.

"Pia wafanyabiashara msikae na fedha nyingi kwa pamoja, kubeba mafurushi ya fedha mkononi siyo salama," aliasa.


## NOTISI / TANGAZO

**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD, JY AUCTIONEERS CO.LTD, MUDU COMPANY LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, SALEI AUCTION MART LTD** kwa mamlaka tuliyopewa naJamhuriya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SALEHE HAMISI SALEHE | DODOMA | SALEHE HAMISI SALEHE | NYUMBA | MTAA WA MBUYINI KATA WA KIZO – DODOMA | 12/06/2021 NA KUENDELEA |
| 2 | FATMA SAIDYHAMISI | KIJITONYAMA | FATMA SAIDYHAMISI | NYUMBA | TUANGOMA-MWAPEMBA-KWA PINDA | 11/6/2021 NA KUENDELEA |
| 3 | TRAZIAS ISHENGOMA | MBAGALA | TRAZIAS ISHENGOMA | NYUMBA | MBAGALA MWANAMTOTI | 12/6/2021 NA KUENDELEA |
| 4 | ROBERT CHACHA NYAMBARI | UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | KITUNDA MTAA KINYANTIRA | 9/06/2021 NA KUENDELEA |
| 5 | ADAM SHABAN KAUNGO | UKONGA | ADAM SHABAN KAUNGO | NYUMBA | MAJOHE- KAUGO | 10/06/2021 NA KUENDELEA |
| 6 | ZEPHANIA PAUL MASANGU | MWANZA | ZEPHANIA PAUL MASANGU | BOMA | NYASAKA CENTRE-MWANZA | 09/06/2021 NA KUENDELEA |
| 7 | FASILI WILLIAM RITTE | MWANZA | FASILI WILLIAM RITTE | NYUMBA | BUJINGWA-BUSWELU | 10/06/2021 NA KUENDELEA |
| 8 | SIKITU HAMIS YAHAYA | MWANZA | HAJI ABEID KASUBI | NYUMBA | NYASAKA'A' – MWANZA | 09/06/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papohapo baada ya mnada kumalizik ana 75% itakayobaki italazimika kulipwandani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0754497396 / 0752 868742 /0785242219/0743885084**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudishakiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

# Mwinyi ataja sababu Mwenge kutowekwa Makumbusho ya Taifa

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema sababu kuu ya mbio za Mwenge, kuendelea kufanyika nchi nzima kila mwaka, kunatokana na dhana mpya iliyoanza mwaka 1994, kwamba umuhimu wa mbio hizo ugeukie kuchochea shughuli za maendeleo na kujitegemea. Katika simulizi ya kitabu chake kiitwacho 'Mzee Rukhsa. Safari ya Maisha Yangu', Mzee Mwinyi, anasema kati ya hoja zilizoibuka akiwa madarakani, ni kuhusu Mwenge, baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kurejeshwa nchini.

Vyama vya upinzani vilikuja na hoja kuwa mbio za Mwenge zinatumia fedha nyingi, hivyo zisitishwe na uwekwe kwenye Makumbusho ya Taifa. "Baada ya Tanzania kuanzisha mfumo wa vyama vingi vya siasa, ikaja hoja kuwa pengine mbio hizo zimefikia mwisho wake.

"Lakini CCM na serikali yake kwa pamoja waliamua kuwa mbio hizo, lazima ziendelee, ila badala ya kuwa shughuli kwenye chama, ziwe sasa zinaratibiwa na serikali mbili," alisema Mzee Mwinyi.

Anasema akiwa mgeni rasmi kwenye kilele cha mbio hizo, Novemba 7, mwaka 1994 zilizofanyika Mazimbu, mkoani Morogoro, ilikuwa ni kilele cha kuhitimisha ajenda ya mbio hizo, kwamba zililenga kupigania uhuru barani Afrika na zilifanikiwa.

"Kuuzima Mwenge wa Uhuru, Mazimbu mwaka 1994, ilikuwa ishara ya kuhitimisha sehemu ya mapambano ya Mwafrika. Maana kupatikana kwa utawala wa walio wengi nchi Afrika Kusini kwa msingi wa demokrasia ya kweli, kulihitimisha mojawapo ya falsafa ya Mwenge wa Uhuru," anasema Mzee Mwinyi;

"Itakumbukuwa kuwa uchaguzi mkuu wa kwanza baada ya kukomeshwa kwa ubaguzi wa rangi Afrika Kusini, ulifanyika Aprili 27, mwaka 1994, ANC walishindwa kwa asilimia 62 za kura. Rais wa kwanza Mwafrika, Nelsona Mandela akaapishwa..."

Anasema dhana mpya ya mbio za Mwenge, hivi sasa ni kutoa fursa ya kipekee kuwahimiza, kuwahamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo yao kwa njia ya kujitolea, kukusanya nguvu na kuondoa kero badala ya kuisubiri serikali pekee.

"Leo ninapoandika bado ninawashukuru sana marais waliokuja baada yangu, akiwamo Rais wa sasa (hayati) Dk. John Magufuli, kwa kuendeleza mbio hizi," anasema Mzee Mwinyi katika kitabu hicho.



Washtakiwa Goodluck Mbowe (kushoto) na Ally Mtena, wakiwa chini ya ulinzi wa Askari Magereza, kabla ya kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi, kusikilizwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi adai kukuta bangi katika gari lililopata ajali

**Na Kulwa Mzee**

INSPEKTA Msaidizi wa Polisi, Degras, amedai alikamata magunia saba ya bangi ndani ya gari aina ya IST lililopata ajali eneo la Kibaha kwa Mathias.

Shahidi huyo alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati akitoa ushahidi mbele ya Jaji Emmaculate Banzi.

Alidai kwamba Oktoba 15 mwaka 2017, alifika Kibaha kwa Mathias na kulikuta gari hilo likiwa limepata ajali huku likiwa limezungukwa na watu majira ya kati ya saa nne hadi tano usiku.

Shahidi huyo alidai alifanya upekuzi kwenye gari hilo na kukuta magunia saba ya bangi, gunia moja likiwa aina ya 'shangazi kaja'.

Shahidi alidai mahakamani huko kwamba akiliona gari hilo na magunia ya bangi anaweza kuyatambua, hivyo mahakama ilihamia nje kwa ajili ya utambuzi wa vielelezo hivyo.

Inspekta Degras alionyesha bangi hiyo ikiwa kwenye magunia na gari linalodaiwa kukutwa na bangi hiyo.

Alitoa hati ya upekuzi iliyokuwa imeorodhesha magunia hayo na mashahidi walioshuhudia upekuzi.

Alidai Hamisi Mwalizo na Justine Ngala walishuhudia na waliopekuliwa walikuwa mshtakiwa Goodluck Mbowe na Ally Mtena.

Shahidi huyo aliomba kutoa hati ya upekuzi kama kielelezo na Upande wa Utetezi ukiongozwa na Wakili Nehemia Nkoko haukuwa na pingamizi.

Mahakama ilipokea kielelezo hicho cha hati ya upekuzi kutoka kwa shahidi huyo namba tatu wa Upande wa Mashtaka.

Upande wa Jamhuri ulimaliza kumhoji shahidi huyo na kuruhusu Upande wa Utetezi kuhoji.

Wakili Nehemia alimtaka shahidi aseme kama kweli au si kweli kwamba magunia aliyoyakuta Kibaha kwa Mathias na aliyoyakuta jana mahakamani yana tofauti kubwa kimwonekano.

Shahidi alidai ni kweli magunia hayo ya bangi yana tofauti kimwonekano na kwamba alipoyakamata aliyakabidhi kwa Koplo Philemon na hakukuwa na maandishi ya makabidhiano.

## Operesheni sasa yaja kuwaondoa wafugaji hifadhini

**Na Gideon Mwakanosya,** TUNDURU

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk.Damas Ndumbaro, ametangaza operesheni ya kuwaondoa wafugaji waliovamia katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na maeneo mbalimbali yaliyotengwa kwa ajili ya utalii hapa nchini.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Kalulu na Jakika wilayani Tunduru, alipofanya ziara ya kusikiliza kero zao kuhusiana na wanyamapori wanaovamia mashamba na kufanya uharibifu wa mazao wilayani humo.

Dk. Ndumbaro alisema tatizo la wanyama hususani tembo wanaokula mazao ya wakulima limechangiwa na wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye maeneo yasioruhusiwa kisheria, jambo linalosababisha wanyama hao kukimbia.

Kwa mujibu wa Dk. Ndumbaro, serikali imeshatenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za ufugaji, lakini kutokana na kiburi cha fedha wafugaji wanawatumia baadhi ya wenyeviti na watendaji wa serikali za vijiji wasiokuwa waaminifu kukahidi na kupeleka mifugo.

Aidha, Dk. Ndumbaro aliwaonya wenyeviti na watendaji wa vijiji hao kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kupokea fedha na kuruhusu wafugaji kufanya shughuli zao kwenye maeneo ya utalii, kwamba tabia hiyo ni kukiuka sheria za utumishi wa umma.

Vilevile, Waziri Ndumbaro, aliwataka wananchi kuepuka kuishi, kufanya shughuli kwenye hifadhi, kwamba serikali haitahusika kulipa fidia wala kutoa kifuta machozi kwa mtu atakayepoteza maisha, kujeruhiwa na kuharibiwa mazao.

HABARI KITAIFA

# Tembo wazidi kutikisa, mbinu kuwakabili hizi

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANANCHI wa vijiji vya Wilaya ya Namtumbo na Tunduru, mkoani Ruvuma wamepewa mafunzo ya ulinzi wa wanyamapori, namna ya kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu kama tembo.

Mafunzo hayo yametolewa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI).

Akizungumza wakati wa mafunzo ya utatuzi wa migogoro kwa binadamu na wanyamapori, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Dk. Emmanuel Masenga, alisema TAWIRI pia imeandaa mfumo wa kufanya ufuatiliaji kwa askari wote wa hifadhi za jamii ngazi za vijiji.

Alisema mfumo huo unamtaka kila mshiriki wa mafunzo hayo walau kutoa elimu hiyo kwa mwananchi mmoja kila mwezi.

Alisema wananchi hao wa vijiji vya Wilaya ya Namtumbo na Tunduru waliopewa mafunzo ya ulinzi wa wanyamapori na namna ya kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu kama tembo, wanapaswa kuhakikisha wanautumia vizuri ujuzi huo, ili kuilinda jamii inayokabiliwa na uvamizi wa tembo.

Naye Ofisa Wanayamapori Mkuu kutoka Idara ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), Dk. Simon Okudo, alisema kwa kuwa wafugaji wananguvu ya fedha wanasababisha uwapo wa changamoto kubwa ya wanyamapori kuingia kwenye makazi ya wananchi, hivyo serikali inapaswa kuwa makini na kulitazama jambo hilo wakati wa mapambano yake.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu malipo kiduchu ya kifuta jasho pindi wanapoharibiwa mazao, kujeruhiwa, kuuawa na wanyamapori.

Mbali na wananchi kupewa elimu, pia askari walijengewa uwezo na mbinu za utatuzi wa migogoro ya wanyama na binadamu, mbinu za ulinzi wa mazao kwa kutumia uzio wa vitambaa na oil chafu.

Alisema pia mbinu ya uzio wa pilipili na mizinga ya nyuki, tochi zenye mwanga mkali, honi, mabomu ya pilipili na matumizi ya vilipuzi vya fataki.

Awali akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, aliwashauri wataalamu waliopewa mamlaka ya kutafsiri sheria kuangalia uwezekano wa kutumia bajeti zinazotengwa na serikali kuchimba mabwawa kwenye maeneo ya hifadhi ili wanyama waweze kupata huduma hiyo huko.

Mtatiro alisema: "Uzoefu unaonyesha kuwa tembo wengi ambao wamekuwa wakisababisha madhara kwa wananchi hufika kwenye maeneo ya makazi ya watu kwa ajili ya kufuata maji, hivyo badala ya kupanga bajeti ya matumizi ya kutoa vifuta jasho na vifuta machozi kwa waathirika, tukichimba mabwawa kwenye maeneo yao inaweza kuwa suluhisho la matukio hayo."

Aidha, Mtatiro aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kuyatekeleza.

## Waingia matatani kwa kushindwa kumweleza waziri fedha maji zilipo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amelazimika kuwakabidhi mikononi mwa vyombo vya dola viongozi wawili wa jumuiya ya watumiaji maji katika Kijiji cha Berege, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, baada ya kushindwa kumpa majibu kuhusu fedha zilizopo.

Viongozi hao ni Mhasibu, Scolastika Simbangulu na Mwenyekiti, Gideon Chesco, huku akiagiza kuvunjwa kwa jumuiya hiyo baada ya kubainika kukusanya fedha bila kupeleka benki.

Aweso alifikia uamuzi huo juzi baada ya kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu jumuiya hiyo na kumwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo, Jabir Shekimweri, kuunda timu ya kufanya ukaguzi maalum ili kujua hali halisi ya fedha zilizopo.

"Jumuiya hii naivunja mara moja haifai maana imeshajifia tayari, Mkuu wa wilaya, vyombo vya usalama vipo, kama kuna fedha imeliwa basi wahusika wazitapike ili hili liwe funzo kwa jumuiya nyingine zote nchini, na niwakumbushe tu jumuiya hizi hazijaundwa kwa ajili ya kula, na tutazifuatilia zote ili kujua mwenendo wake," alisema.

Aliagiza jumuiya za maji zinazoundwa nchini, kuhakikisha zinakuwa na wataalamu wa mradi na mhasibu ili kusimamia mapato na matumizi ya miradi husika.

Kabla ya kufikiwa uamuzi huo, mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Berege, Elias Mjenda, alisema alipelekwa mhasibu kwa jumuiya hiyo, lakini baadhi ya viongozi wa jumuiya walimkataa na kumweka mtu asiye na taaluma ya uhasibu.

Naye, Charles Luhamo, aliiomba serikali kufanya uchunguzi na hatua zichukuliwe kwa waliohusika.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA,MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

**ISO 9001: 2015 CERTIFIED**

**26 Mei, 2021**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

1. Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) itauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara Jenereta pamoja na vifaa mbalimbali vya ofisi vilivyoko katika ofisi dogo ya Mabibo External Dar es Salaam siku ya Jumatano tarehe 09 Juni, 2021 na ofisi ya Kanda ya Ziwa iliyoko eneo la Buzuruga, Nyakato, Ilemela, Mwanza siku ya Jumatatu tarehe 14 Juni, 2021.

2. Vifaa vitakavyouzwa ni kama ifuatavyo;

| Kundi | Maelezo | Idadi |
|---|---|---|
| Na. 1 | Jenereta - 90KV lililopo TMDA Dar es Salaam | 1 |
| | Jenereta 5KV lililopo TMDA Dar es Salaam | 1 |
| Na. 2 | Vifaa mbalimbali vya ofisi na samani zilizoko TMDA - Dar es Salaam na Mwanza | Mchanganyiko |

**3. Masharti ya Mnada**

(i) Vifaa vyote vitauzwa kama vilivyo mahali vilipo;

(ii) Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia 100 ya thamani ya kifaa alichonunua na atalazimika kuondosha vifaa vyake vyote siku hiyo hiyo ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;

(iii) Vifaa vitakavyopigwa mnada vinaweza kuhakikiwa tarehe 03 na 04 Juni, 2021;

(iv) Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumatano tarehe 09 Juni, 2021 kwa upande wa TMDA –Dar es Salaam na saa nne (04:00) asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 14 Juni, 2021 kwa upande wa TMDA - Mwanza;

(v) Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki na kununua vifaa vilivyotajwa.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba**
**S.L.P 1253, Dodoma**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**
**Simu: +255 222450512/ 2450751/ 2452108**
**Simu bila malipo: 0800110084**
**Parua pepe: info@tmda.go.tz**
**Tovuti: www.tmda.go.tz**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilimo uti wa mgongo itekelezwe kwa vitendo

**KILIO** kikubwa cha wabunge juzi kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo ni kukosekana kwa masoko, kilimo cha kutegemea mvua, mfumo wa stakabadhi ghalani na kukosekana kwa mikopo kwa wakulima wadogo licha ya kuwapo kwa benki ya kilimo.

Wabunge hao walieleza kusikitishwa kwao na ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo, huku mkulima akiendelea kunyonywa, licha ya kufanya kazi kubwa na wanufaika wakiwa wachache, huku kukiwa na jitihada ndogo za kuongeza thamani mazao ya wakulima.

Kilio kingine ni vyama vya ushirika ambavyo havijamsaidia mkulima zaidi ya kumuumiza, kwa kuwa kwa sasa hawatoi pembejeo, na kwamba kuna changamoto kubwa ya wataalamu wanaotosheleza.

Kilio kingine ni cha zao la korosho, ambacho kimeendelea kudorora kutokana na mfumo mpya wa sasa baada ya kuondolewa kwa mfuko wa kuendeleza zao hilo, ambao ulikuwa na fedha na serikali ikazichukua na sasa wakulima wanagharamia utafiti na pembejeo kiasi cha kukatwa Sh. 110 kwa kila kilo moja ya korosho.

Wabunge walisema wakulima wanalima mazao, lakini hakuna masoko na hata wakiuza wanauza kwa bei ya kutupwa ambayo inawaumiza.

Walisema wakulima wanalima ila hawajui watauza wapi, huku wabunge kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini walieleza jinsi mahindi ya wakulima yamekosa soko kiasi cha kutaka mazao mbadala ambayo yatakuwa na uhakika wa masoko.

Sekta ya umwagiliaji ilikuwa Wizara ya Maji na sasa imepelekwa Wizara ya Kilimo, lakini bado mabadiliko yake ni madogo huku bajeti iliyotengwa ilikuwa ni Sh. bilioni 17 na kati yake fedha ya ndani ni Sh. bilioni 3 lakini haikutoka hata shilingi moja.

Aidha, walitaka mfumo wa stakabadhi ghalani kuondolewa kwenye baadhi ya mikoa na mazao kwa kuwa hauna tija yoyote na wakitolea mfano mkoa wa Dodoma haukuwa na ulazima wa mfumo huo.

Wabunge hao walisema pia wakulima wengi wanashindwa kuyafikia masoko kutokana na miundombinu mibovu, ambayo humfanya mkulima mazao yake kuoza kabla ya kuyafikia masoko.

Pia walitaka serikali kuunganisha sekta ya kilimo na viwanda ili kuongeza thamani mazao ya wakulima, ambayo yanazalishwa nchini na kununuliwa na wafanyabiashara wa nje ambao hununua na kuonyesha yametoka kwenye nchi zao na hivyo kushika masoko duniani.


Ni muhimu serikali ikatilia maanani suala la kilimo, kama ni uti wa mgongo na kinategemewa na Watanzania asilimia 65 waishio vijijini, huku bajeti inayotengwa kila mwaka ikiwa ni chini ya asilimia moja yaani asilimia 0.08 ya bajeti kuu.

Pamoja na ufinyu wa bajeti, lakini hakuna namna nchi inaweza kusonga mbele bila kilimo sahihi ambacho kitafungamanishwa na sekta nyingine ili kuongeza thamani ya mazao na kubwa ni kuinua sekta ili kufanyia kazi hoja za wabunge.

Tayari serikali imekuja na vipaumbele saba vya kimkakati kwa mwaka mpya wa fedha, wakiamini ndiyo namna ya kuleta jita kwenye kilimo, hivyo ni muhimu fedha za utekelezaji zipatikane ili mwakani kusiwe na malalamiko mengi kama sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ubunifu kupata fedha uanze vyama vya siasa

**MOJA** ya matatizo ambayo yanavikabili baadhi ya vyama vya siasa ni ukata unaosababisha vishindwe kujiendesha ikiwamo kujiimarisha kwa kujenga ofisi maeneo mbalimbali nchini na hata kuwafikia wanachama wake mikoani.

Ukata huo pia unavikwamisha vyama hivyo kushindwa kufanya siasa endelevu, badala yake vinasubiri kampeni hasa wakati wa uchaguzi.

Mambo hayo wakati mwingine husababisha wagombea wa ubunge, udiwani na hata urais na kuishia njiani kutokana na kukosa fedha.

Wakati baadhi ya vyama vikisota, vingine hufanya shughuli kama kawaida kwa vile vimetimiza masharti ambayo yanaviwezesha kupata ruzuku kutoka serikalini.

Kwa taratibu za kisheria ili chama kipate ruzuku, kinatakiwa kupata kura za ushindi wa angalau asilimia tano ya kura zote pamoja na kuwa na wawakilishi bungeni.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 serikali ilitoa ruzuku kwa vyama vyote vilivyokuwa na usajili wa kudumu, ili kuviwezesha kushiriki katika uchaguzi huo.

Nia hiyo njema ilivurugwa na baadhi ya wanasiasa kwa kula au 'kutia ndani' fedha hizo na kusababisha migogoro ndani ya vyama na hivyo kuifanya serikali kuweka utaratibu maalum wa utoaji wa ruzuku hiyo ambao ndiyo unaotumika sasa ukiangalia suala la ushindi.

Utaratibu huo ni chama kupata kura na ushindi wa angalau asilimia tano ya kura zote pamoja na kuwa na wawakilishi bungeni.

Lakini kwa vingine, imekuwa si rahisi kupata ruzuku hiyo, hali ambayo imesababisha baadhi ya vyama kutofikia vigezo hivyo na kuendelea kuyumba.

Tangu uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, ni vyama vichache ambavyo vimekuwa vikipata matokeo ya kupata ruzuku kwenye matokeo ya uchaguzi na kuviwezesha kupata ruzuku, huku vingine vikibaki kulalama.

Ikumbukwe kuwa ruzuku ya vyama vya siasa ni fedha zinazotolewa kwa ajili ya kusaidia shughuli za uendeshaji wa vyama hivyo ambavyo vimetimiza vigezo vinavyotajwa kisheria.

Ni kweli, ruzuku kwa vyama vya siasa ni muhimu ili kuviwezesha kujiendesha, lakini vile ambavyo havikidhi vigezo, havina budi kuja na mbinu za kuviwezesha kujiendesha.

Vyama hivyo vinatakiwa kujipanga kwa ajili ya kujenga mtandao wa wananchama, wadau mbalimbali wa siasa, kuweka mikakati ya kutafuta fedha kupitia njia halali ili viweze kujiendesha.

Kwenye suala hili la kupata fedha za kujiendesha, si vibaya vyama vikatafuta michango kwa marafiki, kuuza kadi, sare, bendera, vitu vingine vya vyama na kuendesha harambee na kuchangisha fedha.

Hatua hiyo inaweza kupunguza ukata kwenye vyama ambao tangu mwaka 2000 umeendelea kuwapo kutokana na kukosa ruzuku, kwa kutotimiza vigezo vilivyowekwa na serikali.

Viongozi wa vyama visivyo na ruzuku, wanaweza kujifunza kwa vyama vinavyopata, ili hatimaye nao wanufaike kuliko kushindwa kujiendesha kwa sababu ambazo wakati mwingine ziko ndani ya uwezo wao.

Ubunifu wa miradi mbalimbali ndani ya vyama ni hoja ya msingi ili kuvisaidia kuondokana na ukata, hasa kwa kutambua kuwa fedha za serikali zina mahitaji mengi ya muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Fedha hizo ni kodi za wananchi ambazo zina matumizi mengi ikiwamo huduma mbalimbali za jamii kama kugharamia elimu, mikopo kwa elimu ya juu, ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya, reli, barabara na kuendesha serikali.

Ni kweli kuna umuhimu kwa vyama vya siasa kupata ruzuku, ili kujiendesha lakini si kila chama, hivyo ni muhimu viongozi wa vyama husika wakajitahidi kuwa wabunifu wa miradi kuliko kutegemea rukuzu.

HABARI KITAIFA

# RC Chalamila aanza kazi kwa kuwananga wasomi

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Albert Chalamila, ameanza kazi rasmi mkoani humo huku akiwataka wasomi kubadilisha elimu yao waliyoipata shuleni kuwa fedha.

Aliyasema hayo juzi katika kikao cha wafanyakazi wa idara mbalimbali mkoani Mwanza wakiwamo viongozi baada ya kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, John Mongella.

Chalamila alitolea mfano, unakuta mtu amesoma mpaka ngazi ya profesa, lakini anatembea barabarani akizungumza mwenyewe kwamba yeye ni msomi, wakati mfukoni hana kitu.

Alisema elimu nzuri ya mtu ni ile anayoweza kuibadilisha na kuifanya iwe fedha za kumsaidia katika maisha yake na siyo vinginevyo.

Mkuu huyo wa mkoa alisema watu wanatakiwa kutafsiri elimu zao katika maisha ikiwamo kuzibadilisha kuwa fedha ili kuona uthamani wake.

Alitoa mfano kwa baadhi ya wafanyabiashara ambao hawajasoma, lakini wana uwezo mkubwa kifedha kuliko wasomi.

Alisema elimu na akili ni vitu viwili tofauti, mtu anaweza kuwa na elimu, lakini hana akili ama akawa na akili wakati hana elimu ya darasani.

Chalamila baada ya kukabidhiwa ofisi juzi, aliomba wananchi mkoani Mwanza kumpa ushirikiano ili aweze kutimiza majukumu yake pamoja na kuwaletea maendeleo.

Aliongeza kuwa maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona Tanzania inapiga hatua katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo na kwamba wananchi wana nafasi kubwa ya kushiriki katika mchakato huo.



Mbunge wa Nachingwea mkoani Lindi, Dk. Amandus Chinguile (kulia), akikabidhi sehemu ya mifuko 1,800 ya saruji yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 22, kwa madiwani na wakuu wa shule juzi, aliyoinunua kusaidia ujenzi wa madarasa katika sekondari 16 jimboni humo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Balozi Mongella atoa angalizo kuhusu Samia

**Na Christina Mwakangale**

SPIKA wa kwanza wa Bunge la Afrika, Dk. Getrude Mongella, amesema Rais Samia Suluhu Hassan, atazamwe kama 'rais' na si jinsi yake.

Dk. Getrude aliyasema hayo jana kwenye mazungumzo na redio moja nchini, akielezea Siku ya Afrika, ambayo huadhimishwa Mei 25, kila mwaka.

"Sasa hivi Tanzania, dunia, inamwangalia na Afrika nzima. Kuna kitu nisichopenda kukiona, ni kumwangalia kama mwanamke, ni rais."

"Kumwangalia kama mwanamke ni kosa, kama alivyosema yeye mwenyewe, kwamba anaweza kuongoza. Kumekuwa na wanawake walioongoza Congo, kinamama tupo kwenye vita ya kujikomboa," alisema Balozi Mongella.

Balozi Mongella akielezea kuhusu siku hiyo, alisema Waafrika wajiamini kuwa wanaweza na kutegemea vya kwao ili kukuza utamaduni wao, ikiwamo lugha kama vile Kiswahili.

Alisema ili kupata maendeleo endelevu ikiwamo kuwatumia wataalamu wa bara la Afrika kutainua vilivyobuniwa barani, badala ya kutegemea zaidi vilivyotoka nje.

"Lazima tuamini akili zetu, mara nyingi utaona akija mtaalamu wa kizungu anavyohangaika naye, lakini akiwa ni mtaalamu wa kiafrika anaanza kuwa na shaka, kwamba huyu anajua, tusipoamini vyetu tutachelewa kugundua vya kwetu," alisema.

Alisema Afrika ijivunie lugha yake na si kuona kwamba wazungumzaji wa lugha za kigeni ndio walioelimika zaidi.

"Kitu ambacho sikufurahishwa nikiwa spika ni mtu kusema mimi ni mu-anglo phone, franco phone. Lugha ya mtu mwingine, lakini nikongoza bunge mtu anasimama na kusema mbona sisi wa kundi la anglo au franco hujatupa nafasi ya kuzungumza, niliwaambia mimi ni Swahili-phone," alisema Balozi Mongella.

# Waelekezwa REA awamu ya 3

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme vijijini (REA) awamu ya tatu mzunguko wa pili, umeanza huku aliwataka makandarasi kuhakikisha hakuna kijiji hata kimoja kitakachorukwa kwenye maeneo walipopangiwa.

Akizungumza jana jijini hapa na makandarasi 34 wanaotekeleza mradi huo, Waziri Kalemani, alisema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, haitakubali kushuhudia uwepo wa vijiji ambavyo havijaunganishiwa nishati ya umeme ifikapo Desemba mwakani.



Alisema vijiji vyote vinatakiwa kupelekewa umeme na kisirukwe kijiji hata kimoja ndani ya miezi 18 ijayo ya utekelezaji wa mradi huo.

Dk. Kalemani (pichani) alisema katika usambazaji huo makandarasi wanatakiwa kuunganisha umeme hata katika nyumba za tembe, vibanda vya biashara pamoja na maeneo ya kuhifadhia mifugo kama wananchi watahitaji huduma hiyo.

Kadhalika, alisisitiza kuwa serikali haitowafumbia macho makandarasi ambao watashindwa kuwaunganishia umeme wananchi ndani ya siku 14 baada ya kulipia huduma hiyo.

"Nasisitiza ni muhimu wananchi wakaunganishiwa huduma ya umeme ndani ya siku 14 tangu walipolipia. REA na TANESCO (Shirika la Usambazaji Umeme Nchini) mkahakikishe hili linatekelezwa," alibainisha.

Hata hivyo, alisema kutokana na mradi huo kutohusisha ulipaji fidia kwa wananchi ambao sehemu ya maeneo yao yatatumika kupitishia miundombinu ya umeme, makandarasi wanapaswa kutumia busara wakati wa upitishaji wa miundombinu hiyo.


## TAARIFA KWA UMMA



**BW. CHACHA JOHN MWITA**

KAMPUNI YA **TSL TECHNOLOGIES LTD.** YA DAR ES SALAAM INAPENDA KUUTANGAZIA UMA WA WATANZANIA KUWA **BW. CHACHA JOHN MWITA** MWENYE PICHA HAPO JUU ALIYEKUWA **BUSINESS DEVELOPMENT MANAGER** SIO MFANYAKAZI WA KAMPUNI YETU TANGU TAREHE 12/05/2021, NA HIVYO KAMPUNI HAITAHUSIKA NA CHOCHOTE ATAKACHOKIFANYA. ***UTAWALA***

# Sendiga aanza na rushwa

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amewataka watumishi mkoani Iringa kuepuka vitendo vya rushwa badala yake wawajibike katika kazi na kutenda haki kwa kila mtu ili kuendeleza kampeni iliyoanzishwa na mtangulizi wake, Ally Hapi ya kuifanya Iringa kuwa sehemu salama.

Sendiga aliyasema hayo juzi wakati wa kukabidhiana ofisi na aliyekuwa Mkuu wa mkoa huo, Hapi ambaye amehamishiwa Mkoa wa Tabora.

Aliwaomba viongozi wa dini kutoa ushirikiano katika ofisi yake ili kuendeleza amani ya mkoa huo huku akiahidi milango yake kuwa wazi kwa kila mmoja atakayefika ofisini kwa ajili ya kupeana mawazo ya kuendeleza Iringa.

"Watumishi wenzangu tutaendeleza kampeni ya Iringa mpya iliyoanzishwa na Ally Hapi, lakini sisi tutakuwa na kaulimbiu isemayo 'Uwajibikaji rafiki wa maendeleo' hivyo nawaomba tuepuke vitendo vya rushwa bali tukawajibike ili kuwaletea maendeleo wananchi na hapo tutasimama kweli kwenye Iringa mpya," alisema Sendiga.

Kwa upande wake, Hapi alisema kuwa katika kipindi cha miezi 34 aliyokuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, alijitoa sadaka kwa wananchi wanyonge na kuwaomba wasihuzunike bali wazidi kumwombea akawatumikie vyema Watanzania waliopo Mkoa wa Tabora.

"Ndugu zangu niwaambie ukweli, ukiona umepewa dhamana ya uongozi katika umri mdogo wa ujana ujue umepewa mtego mkubwa kwani umri huo unakuwa na mihemko mingi sana na ndio umri ambao unaweza kukutana na vitendo vya rushwa, fitina na majungu ya kila aina, niwaombe wakuu wa wilaya msaidieni huyu mama mpelekeeni mambo ya kweli," alisema.

Aliwashukuru na kuwaaga wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa ushirikiano walioutoa tangu alipoanza majukumu yake ya mkuu wa mkoahuku akiwaomba ushirikiano huo wauoneshe kwa mkuu wa mkoa mpya.

"Iringa niliwabeba mgongoni niliwapenda sana na nilikuwa sehemu ya wananchi ninaondoka nikiwa na mapenzi makubwa na nyie msihuzunike ndugu zangu bali mkaniombee huko ninakoelekea nikayafanye yale mazuri niliyofanya na katika uongozi wangu, kweli kuna watu niliwakwaza naombeni mnisamehe sana mimi ni mwanadamu," alisema Hapi.

Alisema katika uongozi wake ndani ya miezi 34 mkoa umefanya vizuri katika sekta ya elimu, afya, uchumi ukusanyaji wa mapato pamoja na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo huku viporo vilivyobaki akimwomba Sendiga kuvimalizia.

Akizungumza kwa niaba ya wazee wa mkoa huo, Omar Nzowa, alisema kuwa wazee walifarijika na uongozi wa mkuu wa mkoa aliyeondoka na wanamwombea heri na kama kunasehemu aliteleza wamsamehe.

## SUA yaagizwa utafiti kubuni teknolojia kilimo cha kisasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amekiagiza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kufanya utafiti wa kubuni teknolojia rahisi za gharama nafuu zitakazosaidia wakulima kuondokana na jembe la mkono ili kuleta uwiano mzuri wa matumizi ya teknolojia na kuongeza uzalishaji.

Alisema kwa kufanya hivyo watakuwa wamemuenzi kivitendo fikra za Hayati Edward Moringe Sokoine, ambaye alikipigania kwa nguvu zake chuo hicho ili kiweze kukuza uchumi wa wakulima na wafugaji kwa kutumia malighafi wanazozalisha.

Alisema hayo katika hotuba ya ufunguzi wa maadhimisho ya kumbukizi ya 17 la Chuo Kikuu SUA, kwa Hayati Sokoine ambaye alikuwa Waziri Mkuu, kiongozi mahiri na shupavu wa nchi ikiwa ni miaka 37 tangu kifo chake, Aprili 12, 1984.

Waziri Ndaki alisema matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye kilimo na ufugaji yana faida nyingi ikiwamo uzalishaji wa chakula cha kutosha, kuongeza kipato cha mkulima na mfugaji na kuchangia kupunguza umaskini. Alisema kuwa takwimu zinaonyesha asilimia 64 ya wakulima nchini wanatumia kilimo cha jembe la mkono ambacho tija yake ni ndogo.

Kadhalika, alisema sekta ya kilimo ndio msingi muhimu wa uchumi wa Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazotegemea kilimo kwa sababu kitaendelea kuwa na mchango mkubwa kwa uchumi kwa miaka mingi ijayo.

Waziri Ndaki pia alisema ukuaji wa sekta ya kilimo nchini kwa maana ya mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi umekuwa hauendi kwa kasi inayotarajiwa kutokana na matumizi duni ya teknolojia.



Meneja Uhusiano wa Jamii wa Mgodi wa Barrick wa Bulyanhulu, Dk. Zumbi Musiba (kushoto), akiangalia bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali kutoka vijiji 14 vinavyozunguka mgodi huo, walioshiriki katika maonyesho ya wajasiriamali na wawekezaji kwenye Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Nyihogo mjini Kahama na kudhaminiwa na kampuni hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Barrick Bulyamhulu yawezesha wanavijiji kushiriki maonyesho

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

WAJASIRIAMALI zaidi ya 33 kutoka vijiji vinavyozunguka mgodi wa dhahabu wa Barrick Bulyanhulu, uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala mkoani Shinyanga, wanashiriki katika maonyesho ya wawekezaji yanayoendelea mjini Kahama kwa ufadhili wa kampuni hiyo.

Maonyesho hayo yaliyoanza jana na yanatarajiwa kumalizika Mei 30, mwaka huu, yanawakutanisha wajasiriamali kutoka wilaya mbalimbali za mkoa wa Shinyanga na yameandaliwa na Taasisi ya GSI Tanzania iliyopo chini ya Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi(NEEC) Kahama chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Akizungumza kwa niaba ya wajasiriamali wenzake waliowezeshwa na Barrick kushiriki, Albert Makere, anayejishughulisha na ufugaji wa kuku, aliishukuru Barrick Bulyanhulu kwa kuwawezesha kushiriki maonyesho hayo makubwa, ambayo yatawawezesha kujifunza mambo mbalimbali yatakayowawezesha kukuza biashara zao.

"Kupitia maonyesho haya tutaweza kupata fursa ya kuonyesha bidhaa tunazozalisha pia tutaweza kupata elimu ya kufungasha bidhaa, urasimishaji biashara na kufungua fursa zaidi za masoko, tumekuja na bidhaa zaidi ya 100 za kuonyesha," alisema Makere.

Aliongeza kuwa miongoni mwa wajasiriamali waliowezeshwa na Barrick, wanajihusisha na kilimo cha mazao ya nafaka, mboga na matunda, wafugaji wa kuku na nyuki, washonaji wa nguo na kikundi cha Geka kinachoendesha mradi wa kutokomeza mazalia ya mbu wanasababishao malaria.

Meneja wa Uhusiano wa Jamii wa Mgodi wa Barrick wa Bulyanhulu, Dk. Zumbi Musiba, alisema wajasiriamali hao ni sehemu ya shughuli za maendeleo ya mgodi wa Bulyanhulu, ambao wamewezeshwa kupewa elimu ya ujasiriamali na kwa wanaojishughulisha na kilimo wamepatiwa mbegu, mbolea na dawa za kuulia wadudu ili wafanikiwe kuendesha kilimo cha kibiashara.

Aliishukuru Taasisi ya GSI kwa kuandaa maonyesho hayo yanayowakutanisha wajasiriamali na wadau mbalimbali wa sekta ya ukuzaji wa biashara ndogo na kuahidi kuwa mgodi wa Bulyanhulu kupitia sera ya kampuni ya kusaidia shughuli za kijamii (CSR), utaendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kukabiliana na changamoto za kijamii sambamba na kuwezesha wananchi waliopo jirani na shughuli zake.

HABARI KITAIFA

# CCM yampa tano Katibu Mkuu wake

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimempongeza Katibu Mkuu wake, Daniel Chongolo, kwa kuanza kutoa mwelekeo na dira ya majukumu ya Sekretarieti ya NEC katika kuisimamia na kufuatilia utendaji wa serikali utakaoleta tija na manufaa kwa umma.

**Yupo tayari kushirikiana na wenzake, lakini atakuwa tayari kupokea na kujifunza, kupokea ushauri na miongozo.**

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, aliyasema hayo wakati wa makabidhiano na aliyekuwa Katibu wa Idara hiyo, Humphrey Polepole.

Shaka alisema yupo tayari kushirikiana na wenzake, lakini atakuwa tayari kupokea na kujifunza, kupokea ushauri na miongozo.

Aidha, alizitaka taasisi za umma na za serikali kutimiza wajibu wake kwa kutumikia na kufuata miongozo ya kisera na malengo ya kimkakati yaliyoainishwa kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM.

Alisema Rais Samia ana nia ya dhati na amedhamiria kujenga nchi, huku akitaka iende kwa mwendo wa haraka, ndiyo maana ameanza kufungua milango.

"Kwa dhamana nilionayo naahidi kuwa kiungo na daraja kwa watendaji wenzangu na makundi ya wanahabari, wanamichezo, wasanii na walemavu. Rais Samia ameshasema upepo uwe mwingi au kidogo jahazi litatia nanga katika bandari ya mafanikio," alisema Shaka.

Shaka alisema Sekretarieti ya NEC haitakuwa tayari kuona Watanzania wakihangaika, kutaabika na kukosa aidha haki za msingi, au kufanyiwa dharau na udhalilishaji wa aina yoyote.

## Wateja Tigo sasa kuwania mil. 200/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania, imezindua promosheni mpya ya 'Testi Zali', Watanzania wataweza kujaribu bahati zao, kujishindia fedha kupitia bahati nasibu.

Kampuni hiyo imesema promosheni hii itawawezesha wateja wa Tigo Tanzania kushinda kwa mara ya kwanza fedha nyingi zaidi, ambapo mshindi kwenye droo kubwa ataondoka na Sh. milioni 200, huku wengine wakijishindia fedha mbalimbali.

Akizungumza jana katika uzindizi wa promosheni hiyo, Mtaalamu wa Huduma za Kidijitali wa Tigo, Ikunda Ngowi, alisema wateja wanaweza kujisajili kupitia (SMS) na kushiriki mara kwa mara kwa ajili ya kushinda zawadi za pesa za papo hapo, pia kuingia kwenye droo kubwa ya bahati nasibu.

Testi Zali itatoa fursa kwa wateja kununua tiketi kwa urahisi na kuangalia kama wamejishindia zawadi ya fedha papo hapo na kujiongezea pointi za kuingia kwenye droo kubwa.

Promosheni hiyo ilitangazwa juzi na itaendelea hadi atakapopatikana mshindi wa Sh. milioni 200 kwenye droo kubwa.

"Tunatarajia kupata washindi 34,884 kila siku, kila wiki ambao watajishindia fedha zaidi ya Sh. milioni 645. Tumekuwa na ubunifu kila wakati, tumekuja na promosheni hii ya kusisimua ambayo itahusisha wateja wetu moja kwa moja na Tanzania kwa ujumla.

"Alisema wateja watakuwa wakijiongezea pointi za kuingia katika droo kubwa ya bahati nasibu ya Sh. milioni 200 ambayo ni ya kwanza nchini.

"Tunaamini itaongeza msisimko na tunatarajia kuwazawadia wateja wetu waaminifu hadi mwisho, ambao wanachangia ukuaji na mafanikio ya kampuni ya Tigo," alisema Ikunda.

Katika promosheni ya Testi Zali, alisema mteja anaweza kutuma ujumbe mfupi kwenda namba (15305), au kutumia menu ya Tigo (*147*00#), au (*148*00#).




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar Es Salaam juzi, wakati wa uzinduzi wa promosheni mpya ya 'Testi Zali', ambapo mshindi wa droo kubwa ataibuka na zawadi ya Sh. milioni 200. Kushoto ni Mtaalamu wa Huduma za Ziada wa Tigo, Ikunda Ngowi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wamiliki viwanda vya chuma watakiwa kutafuta teknolojia

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imewaagiza wamiliki wa viwanda vya chuma nchini kukutana na kujadiliana, kukubaliana kuhusu teknolojia sahihi ya kuchambua vyuma chakavu ambayo itakuwa na uwezo wa kutambua vitu vyenye milipuko wakati wa kufanya uchakataji wa vyuma hivyo.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, alipofanya ziara katika viwanda vya Fujian Hexingwang na Lodhia Group of Companies vilivyopo Mkuranga kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kuboresha mazingira ya kazi yaliyotolewa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) hivi karibuni.

"Wote wanaofanya biashara zinazohusiana na kuchakata chuma wakae katika kikao cha pamoja watafute teknolojia itakayo tusaidia kugundua malighafi zenye mlipuko ili kuepuka ajali zinasababishwa na uchambuzi usiofaa wa malighafi ya viwanda hali ambavyo inasababisha kutokea ajali nyingi ambazo baadhi yake zimekuwa zikigharimu uhai wa Watanzania wenzetu," alisema Naibu Waziri Katabi.

Kwenye ziara hiyo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema lengo la ziara hiyo ni kufuatilia maagizo yalitolewa na OSHA.

Alisema, pamoja na wamiliki wa kiwanda hicho kupewa maelekezo juu ya kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi baada ya tukio la ajali kutokea na kugharimu maisha ya wafanyakazi lakini bado kiwanda hicho hakijatekeleza kwa kiwango kikubwa.

"Tumekuja kuangalia utekelezaji wa maagizo tuliyoyatoa ili tufungue kiwanda hiki kiendelee na shughuli zake, lakini bado hawajatekeleza na sababu ya kutotekeleza tumebaini ni wamiliki wa viwanda kuwa na uelewa mdogo kuhusiana na mambo tuliyowaelekeza," alisema Mwenda.

Alisema OSHA kwasasa inafanya ukaguzi wa kisekta kwa kuzingatia hali ya vihatarishi vya kiusalama na afya.

Nao wafanyakazi wa kiwanda cha Fujian Hexingwang walieleza kutofurahishwa kwao na namna ambavyo mwajiri wao alivyoshindwa kuendesha shughuli kwa kuzingatia sheria za nchi.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Ramadhani Mdimu alisema: "Haipendezi kuona mwekezaji kama huyu anakiuka sheria na miongozo mbalimbali anayopewa na mamlaka mbalimbali za serikali jambo ambalo linasababisha hata sisi wafanyakazi kukosa haki zetu za msingi ikiwamo kufanya kazi katika mazingira salama."

## Tathmini ya kusamehe kodi za nyuma endelevu

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inaendelea kutathmini maombi ya kusamehe kodi za miaka ya nyuma kutoka taasisi mbalimbali, ikiwamo za dini ili kuona hatua za kuchukuliwa bila kuathiri matakwa ya sheria zilizopo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali haioni umuhimu wa kuzisamehe kodi za miaka ya nyuma taasisi za dini zilizokuwa zikiendeshwa kwa utaratibu usiolenga kupata faida na kuziwekea utaratibu taasisi hizo kuanza kulipa tangu walipojulishwa utaratibu wa kuanza kulipa kodi.

Dk. Nchemba akijibu swali hilo, alisema kwa mujibu wa sheria za kodi, taasisi za dini ambazo zinajiendesha kutokana na sadaka kutoka kwa waumini ama misaada inayotolewa na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi hazitakiwi kulipa kodi ya mapato kisheria, isipokuwa taasisi zenye sifa hizo husajiliwa na kupewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN).

Alisema madhumuni ni kuziwezesha kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusu Mamlaka ya Mapato kama vile kuwasilisha kodi zilizokatwa kutoka kwa watumishi na taasisi hizo na usajili wa mali mbalimbali.

Aidha, alisema taasisi za dini zinazofanya shughuli za kiuchumi kwa lengo la kujipatia faida kutokana na shughuli hizo, zinatakiwa kusajiliwa Mamlaka ya Mapato kama wafanyabiashara wengine na kulipa kodi ya mapato kulingana na faida inayopatikana.

"Serikali imekuwa ikipokea maombi ya kusamehe kodi za miaka ya nyuma toka taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi za dini. Serikali inaendelea kutathmini maombi hayo ili kuona hatua zinazoweza kuchukuliwa bila kuathiri matakwa ya sheria zilizopo," alisema.

Aidha, alisema taasisi za dini zinazofanya shughuli za kiuchumi kwa lengo la kujipatia faida kutokana na shughuli hizo, zinatakiwa kusajiliwa Mamlaka ya Mapato kama wafanyabiashara wengine na kulipa kodi ya mapato kulingana na faida inayopatikana.

# Kigezo kikubwa ajira mpya za walimu hiki

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameliambia Bunge kuwa kigezo kikubwa kitakachotumika kwenye ajira mpya za walimu zilizotangazwa hivi karibuni ni wanaojitolea.

Hata hivyo, amesema kuna malalamiko wanaojitolewa wamepeleka barua feki.

Ummy alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akitoa majibu ya nyongeza katika swali la Mbunge wa Longido (CCM), Dk. Steven Kiruswa.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali haioni umuhimu wa kuajiri wa walimu waliojitolea kwenye maeneo wanayojitolea badala ya kuwapangia maeneo mengine.

Ummy alikiri hicho ndio kigezo kikubwa na kwamba kutokana na wengine kuwasilisha barua feki, suala hilo kwa sasa ni tete.

"Jana tumepokea maelekezo yako Mheshimiwa Spika suala hili ni tete nafasi ni 6,949 hadi juzi walioomba ni 89,958, kwa hiyo suala hili Mheshimiwa Spika naomba mtuamini serikali tutatenda haki na hata hao wanaojitolea tutawachambua kama kweli wanajitolea," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna walimu wamehitimu mwaka 2012 hadi 2015 hawajaajiriwa na upo mtazamo ndani ya wizara kwamba waangalie hao waliohitimu siku nyingi kwasababu muda wao wa kuajiriwa serikalini unapungua.

"Suala hili ni tete wenye vigezo ni wengi na nafasi ni chache, lakini tutatenda haki kama ulivyoelekeza bila upendeleo wowote," alisema.

Awali, akijibu swali la mbunge huyo, Naibu Waziri, David Silinde, alisema serikali ilitamani walimu hao wanaojitolea waajiriwe kwenye shule hizo lakini inashindikana kutokana na uhaba uliopo.

"Kwa mfano sasa hivi tuliomba taarifa ya walimu wote wanaojitolea, tukaletewa orodha ya walimu 70,000 na nafasi zilizotangazwa na serikali ni 6,000 utaweza kuona ni changamoto kiasi gani tunapitia katika kukabiliana na janga hilo, serikali itaendelea kuajiri walimu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na kila mwaka tutafanya hivyo ili kupunguza uhaba uliopo," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantum Zodo, alisema kada ya elimu inakadiriwa kuwa na upungufu wa walimu takribani 60,000.

"Je, serikali ina mpango gani wa haraka kukabiliana na changamoto hiyo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema mpango wa serikali ni kuendelea kuajiri na kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa walimu waliokoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kama vile kufariki, kustaafu na waliachishwa kazi kwa mashauri mbalimbali ya kinidhamu.

Aidha, alisema mwezi Mei, 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetangaza ajira 6,949 za walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ili kukabiliana na uhaba wa walimu.

"Serikali itaendelea kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari nchini kadri ya upatikanaji wa fedha," alisema.



Baadhi ya wabunge wakiingia Bungeni, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa tatu katika kikao cha 36 cha Bunge la 12. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Halmashauri zenye hati chafu zaombewa nafuu

BUNGE limeishauri serikali kuangalia upya utaratibu wa kutopeleka fedha za maendeleo kwa halmashauri zenye hati chafu kwa kuwa utawatesa wananchi.

Spika Job Ndugai aliyasema hayo kufuatia swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christine Mnzava.

Ndugai alisema hatua ya kutopeleka fedha za maendeleo kwenye halmashauri kwa kigezo cha hati chafu ni kunyima haki wananchi kwa makosa ya watendaji.

"Lakini ni vyema utaratibu wa kuzinyima fedha sijui halmashauri zenye hati zenye mashaka, sijui hati chafu uangaliwe upya, mfano Mkoa wa Dodoma halmashauri zote isipokuwa halmashauri ya Jiji, Singida halmashauri zote isipokuwa manispaa, Mkoa wa Tabora halmashauri zake zote isipokuwa manispaa zote hizi hazipelekewi fedha," alisema.

Aliongeza: "Utawatesa wananchi wakati ambaye hakuwasilisha vocha ni mhasibu, tupeleke fedha za maendeleo lakini mkiwachukulia hatua watendaji, serikali mliangalie ukipeleka hela acha ifanye kazi."

Alitolea mfano kuwa mwezi huu inapelekwa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari na mambo ya manunuzi yalivyo, lakini Hazina inasubiri kuandikiwa barua kuchelewa kutumia fedha wakati yenyewe ndio imechelewesha kupeleka.


Katika swali la msingi, Dk.Mnzava alitaka kujua serikali itazirejesha lini fedha za ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Msalala zilizorudishwa na mfumo baada ya mwaka wa fedha 2019/20 kuisha.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ilipatiwa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri.

Alisema hadi Juni 30, mwaka 2020, halmashauri hiyo ilikuwa imetumia Sh. milioni 22.4 pekee na hivyo Sh. milioni 477.59 zilirejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2015.

"Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Msalala Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali," alisema.


Alisema serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha za ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa awamu hadi ujenzi wa hospitali hiyo utakapokamilika.





Habari zote na Augusta Njoji

CCM YA SIASA SAFI

Ukurasa 13



Ukurasa 14




# siasa

JUMATANO MEI 26, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


YAHYA SINWAR

# 'Rada' ya Raza... (2)

- Ndivyo ubinafsi ulivyoiua katiba mpya
- Z'bar kuingia OIC ilikuwa njaa si dini



Mohamed Raza akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Mwandishi Wetu**

"NDIYO yenu iwe kweli na hapana yenu iwe hapana, si vinginevyo."

Ni angalizo analotoa Mohamed Raza, mfanyabiashara na mwanasiasa wa Zanzibar, kusimamia ukweli, kufanya yale wanayosema na si kusema 'ndiyo' wakati moyoni wanaloazimia ni 'hapana.'

Raza ambaye alianza kutoa maoni yake kisiasa, kiuchumi na kijamii tangu wiki iliyopita, kwenye Nipashe, anawakumbusha viongozi wanaounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), kuwa wakweli.

Anawataka viongozi wa SUK wa pande zote mbili CCM na ACT -Wazalendo kuwa wakweli katika kujenga Zanzibar mpya na kuwafanya Wazanzibari waone kweli kinachosemwa na kinachotendwa.

"Tuweni wakweli katika kujenga Zanzibar kwa misingi ya makubaliano. Tunayokubaliana tuyatende. Isiwe tunasema lakini upande mmoja unakubaliana kwenye mipango lakini katika utekelezaji unasema hili hatutalitekeleza. Naomba nisema Zanzibar tulipofikia tusirudi tena nyuma."

Anasema zama za uhasama zimekwisha na sasa ni kujenga Zanzibar mpya. Watu wasiangalie nyuma ili taifa lisonge mbele. Hilo litafanikiwa kwa viongozi kuwa wakweli, wanaotenda waliyokubaliana na wanaomuogopa Mungu.

Aidha, anamsifu Rais Hussein Mwinyi kwa kufuatilia utendaji serikalini na kubaini kasoro zilizokuwapo na kushughulikia tuhuma za ufisadi kwa haki.

Utafiti wa Nipashe umebaini kuwa baadhi ya tuhuma za ufisadi na rushwa kubwa zilizoibuliwa na SMZ ni pamoja na sakata la ununuzi wa meli ya MV Mapinduzi II, ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume, ukarabati wa jengo la kihistoria la Beit al Ajab na malipo hewa kwenye vikosi vya SMZ .

Kwa upande wa Rais Samia Suluhu Hassan, Raza anasema hatua anazochukua sasa zinaonyesha kuwa aliona kuwa vitu vingi vinakosekana na sasa anarekebisha akianza na suala la kodi ambalo mamlaka zilikosolewa kwenye kukusanya mapato sasa wafanyabiashara wanaanza kupata nafuu.

"Napenda niwaambie wafanyabiashara wajue kuwa kutoa kodi ni jambo jema kwani zinakwenda kwa wananchi wetu. Ikibidi watoe zaidi . Tubadilike na kulipa kodi bila shuruti ili kuwezesha taifa lipate fedha za kufanikisha miradi ya maendeleo ya nchi yetu," anasema.

**KATIBA MPYA**

Raza anazungumzia katiba mpya ambayo alikuwa mjumbe wa Bunge la Katiba lililokutana Dodoma 2014, akiingia kwa mlango wa Baraza la Wawakilishi.

Anakumbusha kuwa Tanzania imekosa katiba mpya kwa sababu wajumbe hawakuwa wakweli na maslahi binafsi yaliutawala mchakato wote.

Anakumbusha: "Tulikuwa na msimamo nami ni miongoni mwa waliotimuliwa kwa sababu nilibaki na msimamo wangu." Anasema lakini bila kueleza ulihusu nini.

Anasema 'umimi' na 'ubinafsi' ulitawala maamuzi na kwamba kama ubinafsi utaendelea ndani ya chama na serikali si rahisi kufanikiwa kwenye mipango na malengo ya kupata katiba hiyo.

"Msimamo wangu ni huu. Turudi kwenye maoni ya wananchi. Tusiogope katiba siyo msahafu usiobadilishwa. Hii tunaibadilisha (any time) wakati wowote, lakini tunafanya hivyo kwa manufaa ya wananchi wetu. Watanzania Bara na Wazanzibari na si kwa manufaa ya kikundi, kundi dogo au kiongozi."

Anaongeza kuwa kuandaa katiba mpya kufanywe kwa manufaa ya taifa na si vinginevyo akipendekeza kurejea kwenye maoni ya wananchi.

**KUJIUNGA NA OIC**

Raza aliyekuwa mshauri wa Rais Salmin Amour, kwenye mambo ya michezo, katika awamu ya tano, SMZ ilijiunga na Umoja wa Nchi za Kiislam (OIC) na kuzua mjadala mkubwa uliodai kuwa Zanzibar inaelekea kuvunja Muungano baada ya kujiamulia kujiunga na taasisi hiyo ya kimataifa bila kuishirikisha Serikali ya Muungano.

Anapokumbushia mchakato huo, Raza anasema Salmin ni kiongozi wa Zanzibar ambaye baada ya Sheikh Abeid Amani Karume, ni rais aliyepata wakati mgumu mno kuliko yeyote aliyeongoza baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, ndiyo maana katika kutatua matatizo aliamua Zanzibar iingie OIC.

Anasema shida alizopitia zilikuwa kubwa mno 'njaa ilikuwa kubwa'. Na hilo lilitokea baada ya kukosa misaada na nchi kuwa katika hali mbaya kifedha na kiuchumi jambo lililosababisha kutumia juhudi zaidi ili kupata fedha za kusaidia Wazanzibari.

Raza anasema: "Kujiunga na OIC siyo suala la Uislam bali ni kutafuta fedha. Kuna mataifa wanachama wa umoja huo ambao si nchi za Kiislam mfano Uganda, Msumbiji na Burkina Faso na wakati hayo yakitokea marais wa Zanzibar Amani Abeid Karume na Dk. Ali Mohamed Shein wali-

INAENDELEA UK. 12



Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Rais Felix Tshisekedi wa Congo, nchi yake ni moja ya mataifa yenye changamoto kubwa za kiuchumi na amani. **PICHA: MTANDAO**

## SIKU YA AFRIKA

# Bara linapoadhimishwa kwa machungu, corona

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI dunia ikiikumbuka Siku ya Afrika ambayo huadhimishwa kila mwaka Mei 25, mataifa ya bara hilo yanaisherehekea yakabiliwa na hali mbaya kutokana na kuelemewa na umaskini.

Baadhi ya mataifa hayo licha ya kupata uhuru miaka takribani 60 sasa yanashindwa kupiga hatua za maendeleo kutokana na sababu nyingi kama vita vya wenyewe kwa wenyewe na migogoro ya kisiasa iliyodumu kwa miongo mingi.

Matatizo mengine ni uongozi mbaya, ubadhirifu wa mali ya umma, unyanyasaji na uvunjaji wa haki za binadamu.

Spika wa kwanza wa Bunge la Afrika, Dk. Gertrude Mongella, akizungumza katika kuadhimisha siku hiyo, kwenye mahojiano jana na vyombo vya habari, anasema kwa miaka mingi nchi za Afrika, zilijikita kwenye kujikomboa kutoka kwenye makucha ya wakoloni hadi miaka ya 1990, bara zima lilipokuwa huru.

Anasema harakati za ukombozi wa kupata uhuru kwa mataifa mengi, zilianza miaka ya 1950 hadi miaka 1990 na kuanzia hapo mataifa mengi yakajielekeza kwenye kujitafutia maendeleo ya kiuchumi.

Licha ya mafanikio hayo bado kujikomboa kiuchumi ambayo ni hatua Afrika inayoendelea nayo na inayohitajika kupigana kwa nguvu zote anasema Mongella.

Anaeleza kuwa kwa sababu Bara la Afrika halikuumbwa ili litawaliwe na wengine ni lazima kujitahidi kujikomboa kiuchumi na kisiasa licha ya kukumbusha kuwa Afrika iligawanywa, ikatawaliwa kwa sababu ya kupora rasilimali nyingi zilizoko.

"Mizizi iliyowekwa kwa karne, kwamba sisi ni kwa ajili ya kuchukuliwa mali zetu, kwa sababu bara hili ambalo ni tajiri kwa kila hali bado ipo. Katika kuangalia siasa zake naweza kusema ni ngumu. Hata kiuchumi bado ina hali ngumu..." anasema Dk. Getrude Mongella.

Anasema kuna haja ya kuchukua hatua na kuwataka viongozi wa bara la Afrika kusimamia rasilimali zake, ili zinufaishe wananchi na kwamba dhana hiyo inapaswa kueleweka kwa vizazi vyote.

> "Mizizi iliyowekwa kwa karne, kwamba sisi ni kwa ajili ya kuchukuliwa mali zetu, kwa sababu bara hili ambalo ni tajiri kwa kila hali bado ipo. Katika kuangalia siasa zake naweza kusema ni ngumu. Hata kiuchumi bado ina hali ngumu..." anasema Dk. Getrude Mongella.

Mama Mongella ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Wanawake wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Beijing mwaka 1995, anashauri siasa ya kujenga uchumi na kulinda rasilimali za nchi ndicho kiwe kipaumbele.

"Siasa ya kujenga uchumi, kusema chetu ni chetu, ni suala kubwa. Inahitaji uchambuzi wa kina ili kufikia tunapopataka kwenda," anasema Mongella.

Kuhusu, uongozi barani Afrika, anasema bara linaweza kujiongoza na kwamba lilianza kufanya hivyo tangu zamani kwa kutumia uongozi wa kimila na kitamaduni na jamii ziliwaheshimu na zilisonga mbele.

"Uongozi tangu enzi za mababu ulikuwa na mifumo yao ya kujiongoza, ilikuja kuharibiwa wakati tumeanza kutawaliwa. Uongozi bora unahitajika na tunaweza kujiongoza, kabla ya vita ya kujikomboa walikuwapo kina Mkwawa, Kinjeketile, wote wapo kwenye historia," anakumbusha Balozi Mongella.

### UN YATOA USHAURI

Katika kuadhimisha siku hiyo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, anawataka wanasiasa washiriki katika mazungumzo jumuishi na endelevu ya kisiasa ili kuondoa mivutano Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa ya UN, inayozungumzia siku hiyo, Katibu Mkuu anasema kati ya mivutano inayotesa bara hilo na kusababisha migogoro ni siasa, akitaja masuala ya uchaguzi na demokrasia kutozingatiwa.

Guterres anasema kwa kutambua kuwa nchi 20 za Afrika zinapanga kufanya uchaguzi mwaka huu na baadhi zinafikiria kuahirisha, anasema hali hiyo itaathiri utulivu na amani.

Katibu mkuu huyo, kwenye ujumbe wake huo pia anakumbushia wito wa kutaka kusitisha mapigano, ili kutoa fursa ya kukabili janga la corona, akipongeza mataifa ambayo tayari yameitikia wito huo.

Anasema vikundi vilivyojihami huko Cameron, Sudan Kusini na Sudan vimeitikia wito na kutangaza kusitisha mapigano.

"Naunga mkono pia wito wa nchi za Afrika wa kutaka amani iwepo majumbani na kutokomeza aina zote za ukatili majumbani, ikiwamo ukatili dhidi ya wanawake na wasichana."

Kuhusu COVID-19, Katibu Mkuu anasema ni masikitiko makubwa kuwa maadhimisho ya Siku ya Afrika yanakuja wakati wa mapambano na janga la gonjwa hilo, hata hivyo anazipongeza nchi hizo kwa kuonyesha uongozi wa kipekee na uratibu dhidi ya corona.

"Umoja wa Afrika (AU) uliunda kikosi kazi na kuandaa mkakati wa kibara na kuteua wajumbe maalum wa kuhamasisha usaidizi wa kimataifa. Baraza la Amani na Usalama la AU nalo limechukua hatua kukabili madhara ya COVID-19 katika utekelezaji wa makubaliano na hatua za maridhiano," anasema Guterres.

# 'Rada' ya Mohamed Raza... (2)

**INATOKA UK. 11**

kuwapo na wakati huo walikuwa manaibu katika serikali ya Salmin.

Anakumbusha kuwa katika awamu ya Salmin Dk. Shein alikuwa Naibu Waziri wa Afya wakati Karume alikuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na kwamba wakati huo walishuhudia vikwazo vikali na vingi na kwamba hata uongozi wa serikali ya Muungano, ulimweleza kuwa wamekatazwa na jumuiya ya kimataifa kuipa Zanzibar misaada.

"SMZ ilijiunga na OIC baada ya kukosa misaada na siyo Uislamu."

Anasema ili kupata ufumbuzi Rais Ali Hassan Mwinyi, aliamua kuwa Zanzibar ijitoe OIC ili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iingie kwenye umoja huo na kwamba hata hivyo hadi leo haijawahi kuwa mwanachama wa umoja huo na sababu hazijulikani.

### KUHUSU YAJAYO

Raza ambaye sasa anasema amekuwa mfanyabiashara anasema ameondoka kwenye siasa na sasa anafanyabiashara za hoteli, kufua nguo kwa mashine, kubeba mizigo kwenye viwanja vya ndege na samani.

Hata hivyo, anasema licha ya kuondolewa kwenye orodha ya wagombea kwenye Jimbo la Uzini kwenye kura za maoni mwaka 2020, hana wasiwasi kwa vile anafahamu kuwa alitolewa kwenye kinyang'anyiro hicho kwa sababu alikuwa mkweli.

Anapoulizwa ana mpango gani mwaka 2025 anasema: "Yajayo yanafurahisha tuombe uhai kwa Mungu." Na kuongeza 'Man proposes God disposes.' Akimaanisha mwanadamu anapanga mipango mingi, lakini Mungu ndiye anayejua mambo yatakavyokuwa.

# CCM YA SIASA SAFI

## ▪Wachambuzi waona nuru mpya
## ▪Juhudi kumaliza uhasama, tofauti



Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

CHAMA Cha Mapinduzi kimeahidi kufanya siasa safi zenye mashiko na kubeba mstakabali wa taifa katika kuwaunganisha Watanzania, bila kujali itikadi za vyama vyao wala tofauti nyingine.

Ni ahadi ya hivi karibuni kutoka Dodoma inayotolewa mbele ya wanahabari na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, na kujinasibu kuwa dhamira ya chama hicho ipo palepale nayo ni kuhakikisha haishiriki siasa za mti kwa macho, piga nikupige, au watu kuhasimiana kwa sababu za kisiasa.

Hatua hiyo iliyotangazwa na katibu huyo, inakwenda sambamba na kuwahimiza wanasiasa nchini, kufungua milango ya utengemano, maelewano na kuendeleza siasa zenye mashiko kwa manufaa ya taifa.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kuzungumza na wana habari tangu ateuliwe kushika nafasi hiyo na kusisitiza, "hivyo tunawahimiza wanasiasa wenzetu, kufungua milango ya utengamano, maelewano na siasa zenye mashiko na mantiki kwa mstakabali wa taifa."

Nipashe inaifuatilia kauli hiyo ya Chongolo kwa kuzungumza na baadhi ya wachambuzi na wadau wa masuala ya kisiasa, ili kupata mitazamo yao kuhusu dhamira ya chama hicho tawala na kikongwe barani Afrika.

Said Msonga, anaanza kwa kusema hatua ambazo CCM imeamua kuzichukua, zinalenga kuwa na tija kwa Watanzania wote na kwamba, ni za kuungwa mkono ili kuimarisha demokrasia nchini pia kuongeza ushirikiano na kumaliza tofauti.

Mshikamano na umoja wa kitaifa ni muhimu katika kudumisha haki na amani, demokrasia na uhuru wa kisiasa, ndivyo Rais Samia Suluhu Hassan, anavyotamani kurejesha meza ya mazungumzo kwa vyama vyote vya siasa, anasema Msonga.

Mchambuzi huyo anasema, miaka mitano iliyopita, uhuru wa vyama vya siasa uligubikwa na sintofahamu iliyotokana na maelekezo ambayo yalisababisha vyama vya siasa vya upinzani kukwama kufanya mikutano ya hadhara.

"Vyama vipo kisheria na vinatakiwa kufanya shughuli za siasa muda wote na siyo kusubiri kipindi fulani, lakini vilizuiliwa na kuwekewa masharti ya kufanya mikutano na kusababisha msuguano na uhasama mkubwa," anasema.

> "Vyama vipo kisheria na vinatakiwa kufanya shughuli za siasa muda wote na siyo kusubiri kipindi fulani, lakini vilizuiliwa na kuwekewa masharti ya kufanya mikutano na kusababisha msuguano na uhasama mkubwa," anasema.

Msonga anakumbusha kuwa mazingira hayo yalisababisha chuki, uhasama wa kisiasa na kwamba hatua ya CCM kuendelea kusimamia dhamira yake ya kuendelea kuwaunganisha Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao ni nzuri.

**RAIA WALIVUMILIA**

"Nianze kwa kuwapongeza wapinzani na wananchi kwa ujumla kwa kuonyesha uvumilivu mkubwa na nimshukuru Mungu, hakutufikia kujenga uhasama au uadui kitaifa," anasema mchambuzi mwingine, Gwandumi Mwakatobe.

Anasema, miaka mitano iliyopita, vyama vya upinzani vilipitia katika wakati mgumu kuanzia kuzuiwa kufanya mikutano ya siasa, sintofahamu nyingi kutofautiana kisiasa na sakata la uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019.

Anasema, zilikuwapo pia dosari katika uchaguzi uchaguzi mkuu wa mwaka jana, lakini wapinzani na wananchi kwa ujumla wameendelea kuwa wavumilivu, hivyo anaona kuna haja ya kuwapongeza.

Mchambuzi huyo anasema, kwa nchi nyingine, tofauti kama hizi huleta hitilafu au huishia kwenye uhasama mkubwa na hata vita vya wenyewe kwa wenyewe, na kwamba Watanzania wasiruhusu hayo yatokee.

Anabainisha kuwa, ni muhimu kutofautisha mitazamo na misimamo tofauti ya kisiasa na uhasama au uadui wa kisiasa, na kwamba wameacha kufanya siasa za kukosoana kistaarabu na "ushindani" wa hoja na sera mbadala, badala yake upinzani unaonekana kama uhasama au uadui.

Katika suala la kutofautiana, anasema ni la kawaida kuanzia kwenye familia, ndugu na hata marafiki wawili hutofautiana na kuishia kujenga uadui badala ya utengemano na kwamba katika nchi yenye mamilioni ya watu hilo linawezeka.

"Kutofautiana katika mitazamo na misimamo ya kisiasa hakuepukiki kwa taifa lolote lile, lakini pasipo kupata suluhu huweza kugeuka kuwa uhasama au uadui wenye athari kubwa kwa taifa, hivyo suala la maridhiano ni la muhimu kwa mustakabali wa taifa na watu wake," anasema.

Mwakatobe anasema, yale yote ambayo yamechangia kutaka kuleta siasa za piga nikupige na watu kuhasimiana, yapatiwe ufumbuzi wa kudumu ili nchi iendelee kuwa ya amani.

"Tumpe muda na kumuunga mkono katika hayo Rais wetu, si katika kujadili uhasama au uadui, kwani kutofautiana, kupishana au kukosana miongoni mwa watu wengi ni jambo la kawaida, japo kwa viwango tofauti," anasema.

Anafafanua kuwa nchi inaongozwa na serikali ya awamu ya sita ambayo tangu mwanzo imeonyesha kutaka kurejesha demokrasia, wadau wa siasa hawana budi kusaidia kufikia lengo hilo.

"Tumshukuru Mungu Watanzania hatufikia kujenga uhasama au uadui kitaifa. CCM imeahidi kufungua milango ya utengemano, maelewano na siasa zenye mashiko kwa mustakabali wa taifa, isimamie ahadi hiyo," anasema.

**KUJENGA UZALENDO**

Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya, akizungumzia nia ya CCM, anasema, siasa za chuki au za majitaka zimepitwa na wakati zisipewe nafasi katika karne hii kwa kuwa huzalisha ukosefu wa amani, kuondoa utengemano na maelewano. Ni chanzo cha kupumbaza fikra za uzalendo na kuzalisha itikadi kali na za kuchonganisha raia na makabila tena kuibua uhasama.

"Siasa kama hizo hazijengi, badala yake zinabomoa umoja wa kitaifa na hata udungu na kuimarisha uhasama, ambao mwisho wa siku husababisha uasi na visasi kati ya mtu na mtu na hata vyama," anasema Magdalena.

"Kimsingi hakuna anayependa siasa za maji taka, hivyo CCM wasimamie hicho walichoahidi wakianzia kwa kuwazuia makada wao kutoa matamko yanayoashiria chuki na kuvuruga uchaguzi," anasema Sakaya.

# YAHYA SINWAR

## ■Shujaa wa Hamas vita Israel, Palestina
## ■Anayelenga kufuta taifa la Wayahudi

**Na Mwandishi Wetu**



Kiongozi wa Hamas mjini Gaza, Yahya Sinwar, ndiye anayeongoza mapambano baina ya Wapalestina na Israel. **PICHA: MTANDAO**

TANGU kuanza mwezi wa Mei hali ya Mashariki ya Kati, imetatizika kutokana na vita vikali baina ya Israel na wapiganaji wa Hamas kundi linalotetea maslahi ya Wapalestina.

Hamas wenye makazi Ukanda wa Gaza, ina tawi la kisiasa pamoja na tawi la kijeshi, yote mawili yakiwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru na haki za Wapalestina.

Ni kundi lililoanzishwa mwaka 1987, kwa lengo la kupambana na Shirika la Ukombozi la Palestina (PLO) na kwa baadhi ya mataifa linatajwa kama kundi la kigaidi kutokana na kwamba tawi lake la kijeshi mara kwa mara linaishambulia Israel na raia wake ni kwa mujibu wa makala za Sauti ya Ujerumani DW.

Yahya Sinwar, ndiye jemedari wa vita wa wapiganaji wa Kipalestina ambaye amekuwa na nyadhifa za ngazi ya juu kijeshi na kisiasa katika vuguvugu hilo na sasa analiongoza kwenye makao makuu mjini Gaza.

Sinwar, aliyezaliwa mwaka 1962 katika kambi ya wakimbizi ya Khan Yonis iliyopo Gaza, ana historia ya kupigania uhuru na kwa mujibu wa BBC, alikamatwa na kuhukumiwa kifungo cha miaka minne jela mwaka 1988, baada ya kupatikana na hatia ya kuunda kikundi cha al-Jihad cha Da'wah, kikosi cha usalama wa ndani cha Hamas.

Wakati alipoanzisha tawi hili kulikuwa na harakati za kwanza dhidi ya Israel. Hata hivyo, aliachiliwa kutoka gerezani mwaka 2011 wakati Israel ilipokubali kutoa wafungwa wa Kipalestina gerezani ili ipewe mwanajeshi wake, Gilad Shalit, aliyekuwa ametekwa nyara.

Miaka miwili baada ya kuachiliwa, alichaguliwa kuwa mkuu wa ofisi ya Hamas na ilipofika 2015, Marekani iliongeza jina lake kwenye orodha ya magaidi wa kimataifa. Mwaka 2017, alichaguliwa kuwa mkuu wa kikundi cha Hamas Gaza. Na mdogo wake Mohammed Sinwar, au Abu-Ibrahaim, alikuwa kamanda wa kikosi cha Hamas kinachoitwa Al-Qasam Brigade.

Mohamed anasemekana kuwa alishiriki katika kumteka nyara mwanajeshi wa Israel Gilad Shalit, mwaka 2006 na amenusurika majaribio kadhaa ya kumuua kutoka Jeshi la Israeli.

### ASHAMBULIWA

Jeshi la Israel linasema limeilipua kwa bomu nyumba ya kiongozi wa kisiasa wa kundi la wanamgambo wa Kipalestina la Hamas katika mlolongo wa mashambulio ya angani kwenye Ukanda wa Gaza. Ilitoa video ya bomu lililokuwa likilipuka ambalo ilisema liligonga nyumba ya Yahya Sinwar, kiongozi mkuu wa kikundi hicho katika eneo hilo.

Mashambulio ya anga ya Israel huko Gaza yaliwauwa watu wasiopungua 26 Jumapili iliyopita, maofisa huko walisema.

Wanamgambo walirusha roketi zaidi nchini Israel na kupelekea watu kutafuta hifadhi kwingine.

### ALAMA ZA SINWAR

BBC inaeleza baadhi ya sifa zake kuwa kuanzisha kundi la Al-Jihad wa Da'wah - "Majd" kundi la Hamas mwaka 1987 na kuwekeza katika harakati za mwamko dhidi ya Israel lakini 1988 alikamatwa na kufungwa kwa miaka minne gerezani.

Mwaka 2011 - alikuwa mmoja wa Wapalestina 1,027 walioachiliwa na Israel kama sharti la kuachiliwa kwa mwanajeshi Gilad Shalit, ilipofika 2013 alikuwa mjumbe wa vuguvugu la kisiasa la Hamas.

Mwaka 2017 alichaguliwa kuwa Mkuu wa Ofisi ya Siasa ya Hamas katika Ukanda wa Gaza. Aprili mwaka jana aliionya Israel kwamba kama vifaa vya tiba ya virusi vya corona havitatumwa kwenye mwambao wa Gaza, Hamas itachukua vifaa hivyo kwa nguvu na Machi mwaka 2021 alichaguliwa tena kuliongoza vuguvugu la kisiasa la Hamas mjini Gaza.

### VITA NA ISRAEL

Je, Hamas inayopigana na Israel ni kundi gani? Hamas ni kundi kubwa zaidi la waasi linalopigana kwa ajili ya Wapalestina.

Lilianzishwa mwaka 1987 na linafahamika pia kwa jina Harakatul Muqawwamah Al-Islamiyah- jina

> “Wakati alipoanzisha tawi hili kulikuwa na harakati za kwanza dhidi ya Israel. Hata hivyo, aliachiliwa kutoka gerezani mwaka 2011 wakati Israel ilipokubali kutoa wafungwa wa Kipalestina gerezani ili ipewe mwanajeshi wake, Gilad Shalit, aliyekuwa ametekwa nyara.

lake kwa Kiarabu ambalo humaanisha Vuguvugu la Kiislamu na Hamas imeazimia kuiangamiza Israel.

Kundi la wapiganaji wa Hamas ni mojawapo ya makundi kadhaa ya wapiganaji wa Kipalestina ambayo yanadhibiti ukanda wa Gaza, eneo ambalo mara kwa mara hulitumia kushambulia Israel, taifa ambalo halilitambui.

Ghasia mbaya zaidi zilizuka mwezi huu wakati mabomu ya roketi yaliporusha kutoka Gaza kuelekea Israel kwa siku kadhaa huku Israel ikijibu mashambulizi hayo hatua iliyosababisha mauaji na uharibifu kwa pande zote mbili.

Jina lake kwa Kiarabu humaanisha Vuguvugu la Kiislamu na chanzo chake kilianzia siku za kwanza za 'Intifada' au 'mapinduzi ya Palestina' 1987 dhidi ya maeneo yanayokaliwa na Israel katika kingo za magharibi za Mto Yodani (West Bank) na ukanda wa Gaza.

### SHUGHULI KISIASA

Tangu lilipoanzishwa, kundi hilo lina matawi mawili yenye malengo tofauti kwa mujibu wa BBC na kwamba lipo la wapiganaji wa Qassam, linalosimamia mapambano ya kivita dhidi ya Israel ambao uwepo wake haujatumbuliwa na Hamas na upande mwingine kuna 'wingi' ya kisiasa, ambayo lengo lake ni kujenga shule, hospitali na kuisaidia jamii katika masuala ya kisiasa na kidini.

Lakini tangu 2005, lilichukua mwelekeo tofauti, ikiwa ni kuwashirikisha kisiasa watu wa Palestina. Mwaka 2006, Hamas ilichukua utawala baada ya kupata ushindi katika uchaguzi wa bunge la Palestina lakini ushindi wake haukudumu kwa muda mrefu.

Hofu ya kisiasa na kundi jingine la Fatah, ilisababisha kuingia katika mapambano ya kivita

Juni 2007, makundi hayo mawili yalipambana katika vita vikali ndani ya ukanda wa Gaza kabla ya vita hivyo kukamilika huku Hamas likichukua utawala wa ukanda wa Gaza na pinzani wake wa kisiasa Fatah akitawala kutoka 'West Bank'.

Kwa Marekani, Canada, Japan na Muungano wa Ulaya (EU) kundi hilo la Hamas ni la kigaidi kutokana na mashambulizi dhidi ya Israel na lengo lake la kutaka kuliangamizia taifa hilo, kitu kilichoandikwa katika sheria yake.

Lakini kwa wafuasi wake ni vuguvugu halali la kupigania haki za Wapalestina.



# Dk. Mpango kuzindua kampeni ya mazingira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kuzindua kampeni kabambe ya usafi na utunzaji wa mazingira itakayojulikana kwa jina la 'Mazingira yangu, Tanzania yangu naipenda daima' itakayo saidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni hiyo kabambe ya kitaifa.

Jafo alisema kuwa kampeni hiyo itakwenda sambamba na usafi wa mazingira pamoja na zoezi la upandaji miti ikiwa na lengo la kusaidia nchi kukabilina na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema kampeni hiyo inatarajiwa kuzinduliwa Juni 5, mwaka huu, katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani kitakachofanyika kitaifa jijini Dodoma.

"Kampeni hii itazinduliwa na mheshimiwa makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, katika kilele cha siku ya mazingira kitakachofanyika jijini hapa na hii itakuwa ndiyo kampeni kubwa itakayo simamia zile nyingine," alisema Jafo.

Vilevile, alisema kuwa kampeni hiyo inakuja wakati huu ambao nchi inakabiliwa na mabadiliko ya tabia nchi ambayo kwa kiasi kikubwa yamesababishwa na uharibifu wa mazingira hasa katika ukataji miti ovyo.

"Hivi sasa kuna hoteli ambazo zilikuwa zimejengwa katika fukwe mbalimbali hazifanyi kazi tena kina cha maji kimeongezeka kwenye maziwa na bahari kama ile hoteli ya Malaika Mwanza kuna baadhi ya majengo hayafanyi kazi lakini kuna baadhi ya visiwa kule Zanzibar vimemezwa na maji," alisema Jafo.

Alisema kuwa kampeni hiyo itahusisha taasisi zote ikiwamo hoteli, viwanda, migodi mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayojihusisha na masuala ya mazingira.

Alisema kuwa pamoja na kampeni hiyo kuhusisha masuala ya usafi wa mazingira na upandaji miti pia kutakuwa utoaji wa tuzo mbalimbali ikiwamo kwa waandishi wa habari walioripoti masuala ya mazingira.

"Tayari nimeshachagua wajumbe watakaosaidia kuendesha kampeni hii na tutakutana Dodoma Mei 27, mwaka huu, kuweka mambo sawa namna ya kuratibu shughuli mbalimbali," alisema Jafo.

Aidha Jafo, alisema kuwa katika kufanikisha kampeni hiyo tayari imeteua majina 40, ya watu ambao watakuwa mabalozi katika kampeni hiyo kwa kuzingatia nyanja mbalimbali katika jamii ambao watakwenda kuwafikia Watanzania wote.

"Lengo la kampeni hii ni kuifanya nchi kuwa namba moja katika masuala ya utunzaji wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi tunataka watu watoke katika maeneo mengine waje hapa kujifunza," alisisitiza Jafo.

Hata hivyo, alisema kuwa kabla ya uzinduzi wa kampeni hiyo kutakuwapo na mkutano wa maofisa mazingira wote nchini pamoja na mashirika (NGO's) yanayojihusha na masuala ya utunzaji wa mazingira.

# Wasichana 60% hawamudu gharama za taulo za kike

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema asilimia 60 ya wasichana hawamudu gharama za taulo za kike, huku asilimia 28 pekee ndio wenye uelewa juu ya hedhi salama.

Hali hiyo ni matokeo ya utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa hedhi mwaka 2019.

Dk. Gwajima aliyasema jana jijini hapa wakati akitoa tamko kuhusu maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani yatakayofanyika Mei 28, mwaka huu, jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa takwimu hizo zinaonyesha maeneo mengi hapa nchini jamii inakosa uelewa wa umuhimu wa hedhi salama.

Alitaja maeneo yaliyofanyiwa utafiti na kubainika kukosa uelewa wa suala hilo ni Halmashauri ya Namtumbo, Muleba, Mbeya, Igunga, Temeke, Karatu, Tandahimba, Rorya, Kusini Unguja na Kaskazini Pemba.

Alisema wasichana wengi hupata vikwazo vya kumudu gharama za taulo za kike, maji salama na vyoo bora na kutoa wito kwa watengenezaji, wauzaji na wasambazaji wa taulo hizo kuuza kwa bei nafuu ili kumwezesha kila mwanamke au msichana kupata bidhaa hizo kwa urahisi.

"Hivyo, jamii bado inatakiwa kupiga hatua kubwa ya kuendelea kutoa elimu shuleni, katika jamii na pia nyumbani ikiwamo kuwashirikisha kinababa kutambua umuhimu wa hedhi salama kwa ujumla wake," alisema.

Aliagiza kuwekwa kifurushi kwa ajili ya wanafunzi ili kuwapa urahisi na unafuu pindi wanapokuwa kwenye siku zao.

Hata hivyo, alisema wataratibu ajenda ya bei elekezi ya taulo hizo bila kuathiri ubora wake na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya ndani ili kuendelea kulinda bei pamoja na kujihakikishia usalama zaidi wa vifaa hivyo siku zote.

Alitumia fursa hiyo kuwashukuru wadau kupitia mtandao wa wadau wa Hedhi Salama (Menstrual Health and Hygiene (MHH) Coalition) wakiwamo Mashirika ya Kimataifa na ya Kiraia (WB, AMREF, UNICEF, UNFPA,WSSCC, Water Aid, World vision, TAWASANET, AFYA PLUS, DORICAS) na wanachama wake, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI, wanahabari, wenye viwanda vya kutengeneza pedi/taulo za hedhi, wasambazaji, wahamasishaji na watumiaji.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigella (wa pili kulia), akitembelea eneo litakalofanyiwa upanuzi wa kiwanda cha Sukari cha Kilombero, ambao utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 570 na kuongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 127,000 zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani 270,000. Katikati ni Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Guy Williams na Katibu Tawala Mkoa, Mhandisi Emmaneul Kalobero (kushoto) na (kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yachunguza tuhuma udanganyifu fedha za Vodacom

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), mkoani Dodoma, inamchunguza mkazi wa jijini Dar es Salaam, Lyato Bihemo, kwa tuhuma za kufanya udanganyifu na kulipwa Sh. milioni 58.3 na kampuni ya Vodacom na HTT Infranco LTD.

Fedha hizo inasdaiwa amelipwa kama malipo ya kukodisha eneo la kuweka mnara wakati eneo hilo ni msitu wa hifadhi wa Isabe uliopo Halmashauri ya Kondoa mkoani Dodoma.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema uchunguzi umebaini fedha hizo zilipaswa kulipwa kwa serikali ya kijiji au halmashauri. Awali, alifafanua kuwa uchunguzi umeonyesha kwamba mtuhumiwa huyo alisaini mkataba wa ukodishaji wa eneo hilo na Vodacom 2009, kwa kipindi cha miaka 10 na kujifanya mmiliki halali wa eneo hilo.

Katika hatua nyingine, alisema sekta ya ardhi kinara wa vitendo vya rushwa kwa asilimia 15 ya malalamiko yaliyopokelewa na taasisi hiyo tangu Julai 2019 hadi sasa. Kibwengo alisema wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia utendaji wa mabaraza ya ardhi ya kata kwamba yamekuwa ya utendaji unaoashiria vitendo vya rushwa.





# Serikali yawaonya maofisa habari wake

## •Rais Samia atuma ujumbe

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SERIKALI imesema itachukulia hatua kali dhidi ya maofisa habari wa serikali na taasisi zake ambao hawatawajibika ipasavyo kwenye majukumu yao ikiwamo kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya serikali.

Pia imeahidi kutatua matatizo yanayowakabili baadhi ya maofisa hao na kusababisha washindwe kutekeleza majukumu yao ikiwamo ukosefu wa vitendea kazi kama kamera, kompyuta na mtandao wa uhakika.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati alipofungua Mkutano Mkuu wa Chama cha Maofisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali (TAGCO).

Alisema mwelekeo wa serikali ni kuboresha utendaji kazi wa maofisa habari ili kuhakikisha kunakuwa na mawasiliano mazuri kati ya serikali na wananchi kwa kuwawekea mazingira rafiki ya kazi.

"Ninatambua kwamba wapo baadhi ambao mnajituma vizuri kwenye kazi licha ya kutokuwa na vitendea kazi, lakini wapo ambao wana kila kitu lakini hawajitumi, sasa tutaandaa tuzo za maofisa habari wanaofanya kazi vizuri, washindi watapewa motisha na ikiwezekana watapandishwa vyeo, lakini kwa wale wazembe tutashughulika nao," alisema.

Bashungwa alisema serikali itawashughulikia maofisa wengine wa serikali ambao watawakwamisha maofisa habari hao kutekeleza majukumu yao wakiwamo maofisa TEHAMA ambao wamekuwa wakishikilia nywila za intaneti kwenye ofisi zao na kutowaruhusu maofisa habari kuwa na nafasi za kutumia.

Aliwataka viongozi wa serikali wakiwamo wa wizara, mikoa, halmashauri, manispaa na taasisi zote za umma kuhakikisha wanawashirikisha maofisa habari habari kwenye vikao mbalimbali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliiomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuzielekeza halmashauri zote nchini kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya maofisa habari ili watekeleze majukumu yao ipasavyo.

Alisema baadhi ya halmashauri nchini zimekuwa zikiwasahau maofisa hao kwa kutowashirikisha kwenye shughuli muhimu ikiwamo kwenye utekelezaji wa miradi zikiwaona kuwa hawana umuhimu jambo ambalo ni kinyume.

Alisema halmashauri zinatakiwa zitenge bajeti maalum kwa ajili ya maofisa hao kununua vifaa na kupata mafunzo ili wawe na weledi kwenye utendaji kazi wao.

Katika mkutano huo, Rais Samia Suluhu Hassan alituma ujumbe maalum kwa maofisa habari hao akiwataka kufanya kazi kwa weledi ikiwamo kutoficha habari, ujumbe ambao ulisomwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas.

Katika ujumbe huo, Rais Samia aliwataka maofisa hao kuutumia mkutano huo kuhimizana na kuelekezana kuhusu umuhimu wa taarifa na kazi zao. "Yale ambayo ni mazuri ama siyo ya kuridhisha, ni lazima kuwe na namna ya kutoa taarifa kwa umma," Rais Samia alisema katika ujumbe wake huo.

Mkutano huo wa TAGCO umehudhuriwa na maofisa habari, mawasiliano na uhusiano wa serikali 370 kutoka pande zote za Muungano. kati yao, 20 ni kutoka Tanzania Zanzibar.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (kulia), akipeana mkono na Naibu wake, Pauline Gekul kwenye Mti wa Kihistoria unaodaiwa kupandwa na Rais wa Awamu ya Kwanza, Hayati Julius Nyerere kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), juzi. PICHA: NEBART MSOKWA

# LHRC: Ukatili dhidi ya watoto unaongezeka

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

LICHA ya serikali na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kupiga vita vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, vitendo hivyo vinazidi kushamiri katika maeneo mbalimbali nchini na kuuweka hatarini ustawi wa kundi hilo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alibainisha hayo jijini Mbeya jana wakati wa kuhitimisha mafunzo maalum kwa maofisa ustawi wa jamii kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara ya namna ya kukabiliana na kesi zinazohusu ukatili dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

Mafunzo hayo yaliandaliwa kwa ushirikiano kati ya LHRC na Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Idara ya Afya, Maendeleo ya Jamii na Lishe kwa lengo la kuongeza weledi wa usimamizi wa sheria ili kuwalinda watoto.

Alisema ukatili ambao umekuwa ukiripotiwa zaidi dhidi ya watoto ni ubakaji na ulawiti, vitendo ambavyo vimekuwa vikiliathiri kundi hilo katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi huyo alisema ili kukomesha vitendo hivyo, elimu inatakiwa kutolewa katika maeneo mbalimbali ili wananchi wawe na ujasiri wa kutoa taarifa dhidi ya watu wanaohusika na vitendo hivyo na hatua zichukuliwe.

Aliwataka maofisa ustawi wa jamii nchini kuhakikisha wanaongeza bidii ya kutoa elimu kwenye jamii pamoja na kukemea vitendo hivyo vya kinyama ili vikomeshwe.

Vilevile, aliwataka wananchi kuacha kuficha taarifa za unyama huo kwa kukubaliana na wanafamilia na badala yake wawe wanatoa taarifa kwenye vyombo vya dola ili wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria. Vilevile, aliwataka wazazi kuongeza ulinzi kwa watoto wao ili kuwaokoa dhidi ya wabakaji na walawiti huku akisisitiza kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikiwaathiri watoto kimwili na kisaikolojia.

Mwakilishi wa TAMISEMI kwenye mafunzo hayo, Zainab Kitembe, alisema waliamua kuandaa mafunzo hayo ili kuwajengea uwezo maofisa ustawi wa jamii kuwasaidia watoto.

Alisema kwa kawaida watoto huwa hawana uwezo wa kujitetea mahakamani pale wanapokuwa wamekinzana na sheria na hivyo maofisa hao watakuwa wanasimama kwa niaba ya kundi hilo maalum.

Aliwataka maofisa hao kuyatumia vizuri mafunzo hayo kukabili vitendo vya ukatili kwenye jamii huku akisisitiza kuwa serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kupinga ukatili wa aina yoyote.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Selina Mtenya, alisema Idara ya Afya ya Mkoa wa Mbeya, itaendelea kushirikiana na mamlaka zingine katika kutoa ushahidi dhidi ya vitendo vyote vya ukatili dhidi ya makundi yote ya jamii.

# 'Ukilipia malazi, chakula dai risiti'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewataka wageni wote wanaoingia mkoani humo kudai risiti kila wanapopata huduma zikiwamo za malazi, usafiri, urembo na chakula ili kuiwezesha kukusanya mapato kwa ajili ya maendeleo.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, alitoa rai hiyo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Maofisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali (TAGCO) unaofanyika kwa siku nne mkoani humo.

Homera aliwataka wageni hao pamoja na wananchi wote wa mkoa huo kuhakikisha wanapopatiwa huduma wadai risiti za kielektroniki ambazo ndizo zinatakiwa kutumika kwa sasa ili kuepuka kuipotezea serikali mapato.

"Ukipewa risiti hakikisha unafuatilia kilichoandikwa ili ujue kama kiasi cha fedha ulicholipa ndicho kilichoandikwa kwenye risiti hiyo, vinginevyo unaweza ukajikuta unawasaidia wafanyabiashara kuiibia serikali," alisema.

Homera alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo huduma zinazotolewa ni bora na hivyo kila anayeingia anafurahia na kuwa na historia nzuri ya maeneo hayo.

Aliwaalika wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kujitokeza kuwekeza ndani ya mkoa huo kwa maelezo kuwa mazingira ya uwekezaji ni mazuri.



## Rasimu Sera ya Elimu yakamilika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema rasimu ya sera ya elimu imekamilika huku ikijipanga kutumia Sh. bilioni 3.2 kwa ajili ya kuimarisha maabara pamoja na maktaba na kuwawezesha wanafunzi kupata ufaulu kwa kiwango cha juu.

Hayo yalisemwa na waziri huyo, Simai Mohamed Said, wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za wawakilishi waliochangia bajeti ya hotuba yake kwa mwaka wa fedha 2012-2022.

Alisema sera ya elimu ambayo ni moja ya kilio kikubwa cha wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi kwa zaidi ya miaka miwili, imekamilika na ipo katika hatua mbalimbali muhimu kabla ya kuletwa tena kwa wajumbe.

Alikiri kuchukua muda mrefu na kuzitaja sababu zilizosababisha hali hiyo kuwa ni pamoja na kutoa nafasi kwa wadau kuichangia na kutoa maoni yao.

Waziri huyo alisema katika rasimu hiyo suala la mitaala ya masomo kwa wanafunzi ikiwamo wa msingi limezingatiwa kwa sababu ni moja ya malalamiko makubwa ya wajumbe kuhusu kuwapo kwa masomo mengi kwa wanafunzi wa msingi.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba rasimu ya sera ya elimu imekamilika na sasa ipo katika hatua mbalimbali kwa ajili ya kujadiliwa na kuwasilishwa katika taasisi husika... tumechukua muda mrefu kwa ajili ya kutoa maoni kwa wadau," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2012-2022, Wizara ya Elimu, imejipanga vizuri kuimarisha huduma za maabara na kuona kila shule ya sekondari inapata huduma za maabara kwa ajili ya wanafunzi kupata ufaulu mzuri.

Alisema huduma za maktaba zitapatikana katika shule zote za msingi na sekondari pamoja na mawasiliano ya TEHAMA yatakayowawezesha wanafunzi kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

"Hiyo ndiyo mikakati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2012-2022...tunataka kuimarisha huduma za TEHAMA katika shule zote za sekondari kuwawezesha wanafunzi kuingia katika sayansi na teknolojia," alisema.

Wajumbe wamepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara ya elimu kwa mwaka wa fedha 2021-2022 na mawasiliano ya TEHAMA katika shule za sekondari Unguja na Pemba limepewa kipaumbele cha kwanza.

# Viwanda vya dagaa, mwani kuanzishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MCHAKATO wa kuanzishwa viwanda viwili vya kusarifu samaki aina ya dagaa pamoja na kuongeza thamani ya zao la mwani unatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021-2022.

Viwanda hivyo vinatajwa kuwa ni mkombozi kwa wafanyabiashara wadogo pamoja na wazalishaji wa kilimo cha mwani ambao kwa asilimia 80 ni wanawake.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shaaban, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012-2022 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani.

Alisema malengo na mikakati ya serikali ni kuimarisha sekta ya viwanda hatua ambayo itasaidia kuongeza mapato pamoja na ajira kwa vijana.

Shaaban alisema mradi huo unatarajiwa kutekelezwa na sekta binafsi ikiwamo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) pamoja na Taasisi ya Kilimo (TAHA), unatarajiwa kutekelezwa huko Fungurefu na Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema yamekuwapo mafanikio makubwa katika uzalishaji wa samaki aina ya dagaa eneo la Fungurefu na samaki hao wakipata umaarufu mkubwa na soko lake kuimarika.

"Tayari samaki aina ya dagaa wanaozalishwa Fungurefu Mkokotoni, Unguja soko lake la uhakika lipo katika nchi za Afrika ya Mashariki hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya (Congo DRC)," alisema.

"Mheshimiwa Spika mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuimarisha sekta ya viwanda vya aina mbalimbali ikiwamo vidogo ambavyo vitaongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kuingia katika masoko," alisema.

Alisema, ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani kinaendelea huko Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema ujenzi wa kiwanda unaendelea ukiwa katika hatua za kukamilisha ramani na makisio ya kununua vifaa vya ujenzi ambao unafanywa kwa ushirikiano na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), pamoja na kampuni ya Ocean Fresh na Kappa Carrageenan Nusantara kutoka Indonesia.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha kilo 240 za bidhaa ya dagaa na kinatarajiwa kuzalisha mwani na kusarifu jumla ya tani 30,000 kwa mwaka.

Aliwataka wakulima wa mwani Unguja na Pemba kuongeza kasi ya uzalishaji wa kilimo hicho kwa lengo la kukidhi mahitaji na matarajio ya kiwanda.



Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Rahma Kassim Ali (kushoto), akizungumza na Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omar Kheri nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# Kongamano kuzungumzia uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Abdalla Hussein Kombo, amesema serikali imeandaa kongamano kubwa litakalowahusisha wananchi pamoja na wavuvi kufahamu dhana nzima ya uchumi wa bluu na matumizi sahihi ya rasilimali za baharini na kuwanufaisha.

Alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Gavu, aliyetaka kujua lini wizara itawakutanisha wadau wa sekta ya uvuvi na kuwaelezea umuhimu wa dhana ya uchumi wa bluu na kujiweka tayari kunufaika na sekta hiyo.

Alisema serikali imekuja na dhana mpya ya uchumi wa bluu ambao lengo lake kubwa ni kuona wananchi na wadau wa sekta hiyo wananufaika na uchumi huo pamoja na rasilimali za baharini.

Alisema Zanzibar bado haijatumia vizuri rasilimali zinazopatikana baharini ikiwamo kuwawezesha wavuvi kuvua katika eneo la bahari kuu na kuvuna kiwango kikubwa cha samaki kinachopatikana maeneo hayo.

Alisema uvuvi huo umekuwa ukifanywa na wageni pamoja na maharamia kuingia katika maeneo ya ardhi ya bahari ya Zanzibar na kuvuna rasilimali za samaki kinyume na sheria.

Kombo alisema katika kuelekea uchumi huo mazingatio ya sheria za uvuvi ikiwamo kupambana na uvuvi haramu unaoharibu matumbawe, utazingatiwa kwa kiwango kikubwa.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba wizara yangu ipo katika matayarisho ya kongamano kubwa litakalowakusanyisha wadau mbalimbali na kuelezea dhana nzima ya uchumi wa bluu," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**SHERIA YA ARDHI NAMBA 4 YA MWAKA 1999**

**(SURA YA 113)**
**ILANI YA KUHAMISHA JINA LA MMILIKI WA KIPANDE CHA ARDHI**
**NAMBA YA KIWANJA: TMK/MBGK/MGK 14/240**
**JINA LILILOANDIKISHWA: FAKHI HASSANI LINGONI**
**ANAYEOMBA: JOKHA AHMED SEIF**

Ilani inatolewa kwamba kipande cha ardhi kilichotajwa hapo juu kilikuwa kinamilikiwa na **FAKIHI HASSANI LINGONI.** Nakusudia kuhamisha umiliki wa kipande cha ardhi kinachomilikiwa na **FAKIHI HASSANI LINGONI** kutokana na mauziano yalifanyika, ambapo taratibu za uhamisho hazikufuatwa. Taarifa inatolewa kwako ndani ya siku ishirini na nane (28) kuanzia tarehe ya ilani hii na endapo hakuna pingamizi lolote tutaendelea na umilikishaji/uhamisho wa kipande hicho cha ardhi.

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.211/2019**
**ATENY SIAME::::::::::::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**SALUM JERY::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**YAH : KUITWA SHAURINI**
**KWA :**
**SALUM JERY**

Fahamu kwamba **ATENY SIAME** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe **03/06/2021 saa 2:30** asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.

Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe **11/05/2021.**

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**11/05/2021.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.154/2021**

Ombi la **CONSOLATA JACKSON MAGESA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **CELESTINA HENRY CHUMA WA MAFIGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **24/06/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**YUSUPH KASSIM KISWAMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 877 CDY** chasisi namba **LC6PCJK230076562** engine namba **156FM15AD2F46447,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/CEN/RB/261464/2021**

---

ROCK TAKERS LTD

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA MADAI NA 386/2019**
**HERIETH SHISHIRA ................. MDAI**
**DHIDI YA**
**CLIFF GUSTAF TETY .......................MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI NA. 114/2019**

**KAMISHNA WA ARDHI .......................................MDAI**
**DHIDI YA**
**VISHAL SODHA ........................................... MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI NA 01/2020**
**TOGOLAI KOPWE ............................................... MDAI**
**DHIDI YA**
**SANDRA LUGWISHE .......................................MDAIWA**

**KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA, PAMOJA NA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA AMBAZO NI VIWANJA NA MAGARI SIKU YA IJUMAA TAREHE 10/6/2021 NA 11/6/2021. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ZILIPO.**

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | VIWANJA VIWILI (2) | VIWANJA NAMBA 3 NA NAMBA 4, BLOCK "A" ILUNGU, MAGU. | SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA 10/06/2021 |
| 2 | GARI, TOYOTA HARRIER T 906 DQP | VIWANJA VYA FURAHISHA - MWANZA | SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA 11/06/2021 |
| 3 | GARI, NISSAN PICK UP T 219 AHW | VIWANJA VYA FURAHISHA - MWANZA | SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA 11/06/2021 |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATAILIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) , KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0627672221/0659570570**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie**
**0782253676**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rais Mali, Waziri Mkuu washikiliwa na jeshi

**Bamako,** MALI

MAOFISA wa kijeshi wa Mali, wanamshikilia rais na waziri mkuu wake katika kambi ya jeshi.

Rais Bah N'Daw na Waziri Mkuu Moctar Ouane na maofisa hao wanadai hatua hiyo imekuja baada ya kukasirishwa na mabadiliko ya baraza la mawaziri.

Jumuiya ya kimataifa zimelaani vikali na hatua hiyo na kutaka viongozi hao waachiliwe huru.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Ulaya (EU), Marekani na Uingereza imetoa wito wa kuachiliwa huru mara moja.

Kukamatwa kwao viongozi hao wanaoongoza serikali ya mpito, iliyoundwa baada ya mapinduzi ya kijeshi Agosti, kumeongeza hofu ya kutokea mapinduzi mengine.

Viongozi hao walikamatwa baada ya kufanya mabadiliko ya baraza la mawaziri mapema juzi, ili kutuliza ukosoaji mkubwa uliokuwa ukiikabili serikali yao ya mpito. Aidha EU, ulisema uko tayari kuzingatia kuwachukulia hatua viongozi wa kisiasa na kijeshi ambao wanazuia kufanyika mabadiliko nchini Mali.

"Tunalaani kilichotokea Mali, utekaji nyara wa rais na waziri mkuu. Tunaunga mkono ujumbe uliotumwa na SADC na AU," alisema Charles Michel, Rais wa Baraza la Ulaya.

Michel alisema kwa pamoja wanatoa wito wa kurudishwa kwa serikali ya mpito na kwamba klichotokea ni kitu kikubwa na wako tayari kuzingatia kuchukua hatua zinazohitajika.

Matukio hayo yamezua wasiwasi iwapo serikali ya mpito itaweza kuendelea na mipango yake ya kuandaa uchaguzi mpya, kama ilivyoahidi kufanyika Februari, mwakani.

UN, imekuwa ikitumia dola bilioni 1.2 kila mwaka, kuweka ujumbe wake wa askari wa kulinda amani nchini humo.

Viongozi hao wawili, waliapishwa Septemba mwaka jana, baada ya jeshi la mapinduzi kukubali kukabidhi uongozi kwa serikali ya mpito ya kiraia kufuatia shinikizo la kimataifa.

Jeshi lilichukua madaraka mwezi mmoja kabla ya wanajeshi kuizingira nyumba ya Rais Ibrahim Keita na kufyatua risasi hewani.

Keita aliamua kujiuzulu kupitia kituo cha televisheni ya taifa na kusema, hatomwaga damu ili aweze kubakia madarakani.

Wanajeshi walijitangaza katika kituo cha televisheni ya taifa kama Kamati ya Kitaifa ya Ukombozi wa Watu na kuahidi kurudisha haraka utawala wa kiraia.

Hatua ya kuwakamata rais na waziri mkuu wa nchi inaonekana kutia shaka ahadi hiyo.

Kukamatwa kwa viongozi hao, kulitokea saa moja au zaidi, baada ya Baraza la Mawaziri la serikali mpya, kutangazwa na kutowajumuisha Waziri wa Usalama wa Mambo ya Ndani, Modibo Kone au Waziri wa Ulinzi, Sadio Camara, wote wakiwa wanachama wa jeshi la mapinduzi.

Hakuna sababu iliyotolewa kuhusu kutengwa kwao, ingawa hatua hiyo inaashiria kuongezeka kwa mgawanyiko ndani ya serikali ya mpito.

**DW**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken (katikati), akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Gabi Ashkenazi, baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Tel Aviv Ben Gurion, jana, mjini Tel Aviv, nchini Israel. **PICHA: AP**

## Afrika yasherehekea Siku ya Afrika

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

SHEREHE za kuadhimisha Siku ya Afrika, iliyoanzishwa na Umoja wa Afrika (OAU), ambao sasa ni Umoja wa Afrika (AU), zimefanyika katika nchi tofauti barani.

Nchini Zimbabwe, Rais Emmerson Mnangagwa alitarajiwa kuzindua sanamu ya Nehanda Charwe, maarufu Mbuya Nehanda, ambaye aliongoza mapinduzi ya miaka ya 1800.

Muungano wa Afrika umekuwa ukiweka mtandaoni dondoo za kuvutia, kuhusu nchi 55 za wanachama wake.

Nchini Cameroon, muungano huo uliangazia juhudi za mwanaume mmoja mwenye umri wa makamu ambaye ameboresha huduma za afya nchini humo.

Katika ujumbe wake, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa alisisitiza haja ya nchi za Afrika kudhibiti uhuru wao.

"Kama mataifa ya Afrika, tunataka kujisaidia na wala sio kuambiwa ni kitu gani kizuri kwetu. Kanuni ya hakuna chochote kinachotuhusu kitakachojadiliwa bila sisi inapaswa kutumika," alisema Rais Ramaphosa.

**BBC**

## Blinken azuru Mashariki ya Kati

**Tel Aviv,** ISRAEL

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, amefanya ziara Mashariki ya Kati, ili kudumisha amani kati ya Israeli na Hamas.

Siku nne baada ya kusitishwa mapigano kati ya Israel na Hamas, waziri huyo aliwasili, Tel Aviv kuanza ziara ya Mashariki ya Kati ambayo pia itampeleka Palestina, Misri na Jordan.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani, Joe Biden na mwenzake wa Misri, Abdel Fattah al Sisi, wamejadiliana kuhusu makubaliano yaliyosaidia kusitisha mapigano kati ya Israel na kundi la Hamas katika Ukanda wa Gaza, huku mashirika ya kimataifa yakitoa wito kwa misaada ya kibinadamu kuwasaidia wakazi wa eneo hilo baada ya mashambulizi ya Jeshi la Israel.

**RFI**

# Chifu aamuru Mugabe afukuliwe, azikwe upya

**Harare,** ZIMBABWE

KIONGOZI wa kitamaduni Zimbabwe, ameamuru mabaki ya rais wa zamani wa nchi hiyo, Robert Mugabe, yafukuliwe na kuzikwa katika makaburi ya kitaifa.

Mugabe alifariki mwaka 2019 na kuzikwa nyumbani kwake, Kutama, kutokana na ombi lake na wala sio katika makaburi ya mashujaa wa kitaifa katika mji mkuu, Harare, kama alivyotarajia mrithi wake Rais Emmerson Mnangagwa na wengine.

Familia yake ilisema, Mugabe alikuwa ameelezea hofu yake kwamba, mahasimu wake wa kisiasa waliomwondoa madarakani mwaka 2017, huenda wakatumia mabaki yake kufanya kafara, ikiwa atazikwa katika makaburi ya kitaifa.

Siku ya Jumatatu wiki hii, chifu wa kitamaduni katika Wilaya ya Zvimba, Magharibi mwa mji mkuu wa Harare, alisema kwamba amepokea malalamishi kutoka kwa jamaa wa ukoo wa Mugabe, kuhusu mahali alipozikwa.

Aliamua kwamba, Grace Mugabe alikosea kukiuka mwongozo wa kimila kwa kumzika mume wake nyumbani kwake.


Grace, hakufika mbele ya kikao hicho, ingawa chifu alimpiga faini ya kulipa ng'ombe watano na mbuzi mmoja.

"Yeye (chifu) hana mamlaka dhidi ya Kutama. Na hata kama chifu alifanya uamuzi sahihi tungekata rufani mahakamani," alisema Leo Mugabe, msemaji wa familia, akizungumza na shirika la habari la Reuters.

**BBC**

# FORLAN

## AKUNWA NA MAFANIKIO YA CAVANI



**MANCHESTER, England**

MAFANIKIO ya Edinson Cavani pale Manchester United hayajaja kama mshangao kwa mshambuliaji wa zamani wa 'Mashetani Wekundu' hao na Uruguay, Diego Forlan.

Cavani ameng'ara tangu alipojiunga na United kwa uhamisho huru akitokea kwa miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain mwanzoni mwa msimu wa 2020-21 - na matokeo yake akaongezewa tena mwaka mmoja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amefunga mabao 16 kwenye mashindano yote msimu huu, huku akijiandaa kuichezea Man United kwenye fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Villarreal Jumatano hii, wakiwa wamemaliza nafasi ya pili nyuma ya mabingwa Manchester City kwenye Ligi Kuu England.

Forlan, ambye alicheza na Cavani katika kikosi cha Uruguay, amemsifia nyota huyo wa United.

"Edinson Cavani ni mchezaji mkubwa, namjua sana. Tulicheza pamoja kwa miaka mingi katika timu ya taifa, nina furaha kubwa kwa mafanikio yake," alisema Forlan akinukuliwa na Dail Mail.

"Mshangao? Hapana. Hapana, kwa sababu najua uwezo wake na namna anavyocheza. Ni mchezaji wa daraja la juu na mtu mzuri.

"Hivyo sijashangazwa, nilijua kwamba angekuwa mchezaji mwenye ubora kama alionao sasa, na nina furaha kubwa juu yake ataendelea kucheza kwa mwaka mmoja zaidi pale United."

# KANTE, MENDY FITI FAINALI UEFA

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ana matumaini chanya juu ya ufiti wa wachezaji wake, N'Golo Kante na Edouard Mendy kuelekea fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiungo Kante alikaa benchi wakati wakipoteza 2-1 kwa Aston Villa Jumapili wakati Blues wakifanikiwa kumaliza kwenye nne bora katika Ligi Kuu England, shukrani kwa ushindi wa Tottenham Hotspur dhidi ya Leicester City kwenye mechi za funga msimu.

Golikipa Mendy alitolewa nje hapo Villa Park baada ya kuumia mbavu na kumfanya kuwa shakani kwenye fainali hiyo dhidi ya Manchester City jijini Porto Jumamosi iliyopita.

Hata hivyo, Tuchel haoni kama majeraha hayo yanaweza kuwa tatizo kuelekea kwenye maandalizi ya mchezo huo.

"Hali haijabadilika kwa N'Golo kwani bado tunasubiria ufiti wake, lakini anaonekana yuko vizuri na atarudi kwenye mazoezi Jumatano," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari jana, Jumanne.

"Nafikiri kuhusu kubadilisha mbinu zangu, sasa acheni kuuulizia kuhusu N'Golo.

"Nitamwingiza dimbani Jumatano kwenye mazoezi na msiniulize zaidi, kwani tutaona Jumatano (leo).

"(Mendy) ameonyesha kuimarika vizuri zaidi na hana maumivu makubwa sana, hivyo na yeye atakuwa kwenye mazoezi Jumatano (leo).

"Na kama Edou atakuwa fiti kwenye mazoezi Jumatano, nina uhakika kabisa kwamba atacheza fainali hii."




# SUAREZ KUBAKI ATLETICO

**MADRID, Hispania**

LUIS Suarez amethibitisha kabisa kuwa atakaa Atletico Madrid kwa angalau msimu mwingine mmoja, kwa mujibu wa Movistar.

Mshambuliaji huyo alisaini mkataba wa miaka miwili alipojiunga na Atletico kutoka Barcelona msimu uliopita na amekuwa muhimu katika ushindi wa taji la LaLiga, akifunga mabao 21.

"Ndio, nina hakika nitakaa," Suarez aliiambia Movistar.

"Atletico walinikaribisha vizuri tangu dakika ya kwanza nilipofika ... nimefarijika sana jinsi walivyonitendea."

Raia huyo wa Uruguay alionekana akitokwa na machozi akiita familia yake uwanjani huko Valladolid baada ya kushinda LaLiga na Atletico.

"Mke wangu ndiye amekuwa nami kila siku [Atletico]," alisema.

"Ilikuwa ngumu sana msimu uliopita wa majira ya joto, wakati una watoto watatu na maisha ya utulivu. Mateso yalikuwa magumu.

"Mke wangu anajua ni kiasi gani nimefanya kazi kuweza kuendelea kuonyesha kuwa ninaweza kubaki katika kiwango cha juu zaidi.

"Watoto wangu hutumia maisha yao na marafiki zao, shuleni, walijua kuwa ilikuwa mabadiliko kuhamia Atletico."



# RONALDO: NIMEFIKIA MALENGO YANGU JUVE

**TURIN, Italia**

Cristiano Ronaldo amesema kuwa amefanikiwa kwa asilimia kubwa malengo yake akiwa klabu ya Juventus.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Ronaldo ameandika ujumbe mzito juu ya safari yake ya soka akiwa na Juventus na mafanikio aliyoyapata.

Ronaldo ameainisha kuwa sehemu ya msingi ya kupima mafanikio, ni kuanza kutazama kuanzia mtu binafsi na kisha mchango wa kila mmoja anayehusika na klabu katika kufanikisha jambo kwa timu.

Licha ya kushindwa kutetea taji la Serie A msimu huu, Ronaldo amewapongeza Inter Milan kwa jitihada zao na kustahili kutwaa taji hilo. Kwake ni muhimu kutambua mchango wa kila mmoja na timu kwa ujumla.

Akitaja Italian Super Cup, Italian Cup na kuwa mfungaji bora Serie A kwake ni heshima kubwa hasa kwa nchi kama Italia ambayo ni vigumu kushinda kitu chochote.

"Kwa mafanikio haya, nimefikisha malengo ambayo nilijiwekea mimi binafsi tangu siku ya kwanza nilipofika Italia.

"Kushinda Serie A, Super Cup na kuwa mchezaji bora na mfungaji bora kwenye nchi kubwa kisoka yenye wachezaji mashuhuri, klabu kubwa na utamaduni wa kipekee wa soka, ni jambo la muhimu sana kwangu."

Ujumbe wa staa huyu umezua sintofahamu, ingawa hatima yake bado haijawa wazi, huku ikibainishwa kuwa mpango wake ulikuwa kuondoka Juventus ikiwa wangeshindwa kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini Juventus wamefanikiwa kufuzu dakika za mwisho

## RAMOS AKUBALI KUTEMWA HISPANIA KWA EURO 2020

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos amekubali kuondolewa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania kinachokwenda kwenye michuano ya Euro 2020 akieleza ni uamuzi bora ili apumzike.

Nahodha huyo wa Real Madrid, Ramos ndiye mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa kikosi cha Hispania (180), aliachwa na kocha Luis Enrique ambaye alitaja wachezaji 24 kwa ajili ya mashindano hayo yanayoanza mwezi ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, amekuwa akisumbuliwa na majeraha kwa msimu mzima wa 2020-21, akicheza mechi 21 kwa Madrid katika mashindano yote, zote hizo zikija tangu mwishoni mwa Machi.

Hata hivyo, uamuzi wa Enrique kumwondoa Ramos kwenye kikosi hicho, ulizua mshangao mkubwa Jumatatu, huku pia kukiwa hakuna mchezaji yeyote wa Real Madrid.

Lakini wakati kukiwa na mshangao huo kutoka kwa mashabiki wa Madrid, Ramos amesema ni kawaida.

"Baada ya miezi michache na msimu wa ajabu, nilifikiria nitamalizia muda wangu kwenye michuano ya Euro," aliandika Ramos kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Nimepambana na kujifua kila siku kwa asilimia 100 kwa Real Madrid na timu ya taifa, lakini mambo yamekwenda tofauti.

"Inaniumiza kuwa sitakuwapo kwenye timu ya Taifa ya Hispania kuisaidia katika mashindano makubwa, lakini katika hili jambo zuri ni kupumzika."

## RASHFORD KUONDOKA MANCHESTER UNITED

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Marcus Rashford, amekataa kuitupilia mbali nafasi ya kutaka kuondoka Old Trafford katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Rashford mwenye umri wa miaka 23, ameelezea shauku yake ya kuicheza moja ya miamba ya Hispania kati ya Barcelona au Real Madrid pia kutaka kujifunza lugha za kigeni.

"Siwezi kusema hapana, mbali ya Manchester United mimi ni shabiki mkubwa wa Barcelona na Real Madrid, kwa sababu kila siku wana wachezaji wazuri vilevile wanacheza mpira mzuri," alisema akinukuliwa na Sky Sport.

"Kila mtu anaiangalia Real Madrid na Barcelona, na hilo liko wazi pia kwa upande wangu".

Maneno hayo ya Rashaford yameonekana kuzua mjadala mkubwa ukizingatia kumekuwa na rundo kubwa la wachezaji kutoka England waliojiunga na miamba hiyo ya Hispania kwenye siku za karibuni.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA: SIONI ZIDANE AKIONDOKA REAL MADRID

Huku akihusishwa kutimkia Juve, straika huyo amesema hataondoka na ana uhakika kwa hilo...

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid, Karim Benzema, haamini kama Kocha Mkuu, Zinedine Zidane, ataondoka hapo Santiago Bernabeu huku kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa yake.

Zidane anatarajiwa kuondoka Madrid baada ya kipindi cha pili cha kuwanoa miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku klabu yake ya zamani ya Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus akihusishwa nayo.

Baada ya kuisaidia Madrid kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo na taji la LaLiga katika kipindi cha kwanza, Zidane alirudi Madrid mwaka 2019 na alipata taji la LaLiga msimu uliopita.

Hata hivyo, 'Los Blancos' msimu huu walipigwa chini na wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid.

Wakati uvumi huo ukitawala, Benzema ameiliambia Jarida la L'Equipe katika mahojiano maalumu yaliyochapishwa Jumanne: "Simuoni kama anaondoka.

"Hataondoka, nina uhakika na hilo, tutaona."

Madrid ilimaliza msimu wa 2020-21 ikiwa haijafungwa katika mechi 18 (ikishinda 13, sare tano) kwenye LaLiga - ikiwa ni rekodi ya mechi nyingi zaidi ya kutofungwa kwa msimu huu.

Na hiyo ilikuwa nzuri zaidi tangu Machi 2014 chini ya Carlo Ancelotti (ikishinda mechi 15, sare tatu).

Benzema alihusishwa katika mabao 32 kwenye LaLiga msimu huu (mabao 23 na pasi za mwisho tisa), ikiwa ni rekodi bora zaidi kwa msimu mmoja kwake akiifuta ile ya msimu wa 2015-16 (alipohusika na mabao 31, akifunga 24 na pasi za mwisho saba).

Pasi sita za mwisho alizopewa na Rodrygo Goes zikachangia Benzema kufunga mabao hayo kwenye LaLiga.

## KWA UFUPI

**SANCHO ANAWEZA KUONDOKA**

BORUSSIA Dortmund wamemwambia winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, kuwa anaweza kuihama klabu hiyo katika dirisha la usajili la majira haya ya joto. ***(Bild)***

**BALE, HAZARD WAWEKWA SOKONI**

REAL Madrid wako tayari kupokea ofa za timu zitakazotaka kuwasajili winga wa Wales, Gareth Bale mwenye miaka 31, na kiungo mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard, 30. ***(Sky Sports)***

**SPURS KUMUUZA DELE**

KLABU ya Tottenham Hotspur ina mpango wa kumuuza kiungo wao mshambuliaji, Dele Alli mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

**SUAREZ KUBAKI ATLETICO**

LUIS Suarez amesema ataendelea kubaki na mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Atletico Madrid, licha ya kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kutoka Uruguay kuhusishwa na taarifa za kurejea katika klabu ya Liverpool. ***(Liverpool Echo)***

**LINGARD AZUA HOFU USAJILI**

KLABU ya West Ham ina hofu Manchester United watawazuia kumsajili kwa mkataba wa kudumu winga wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

**JUVE KUMUUZA RAMSEY**

JUVENTUS wako tayari kumuuza kiungo wa Wales, Aaron Ramsey, mwenye umri wa miaka 30, kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Calciomercato)***

**BARCA, DEMBELE KUTETA**

BARCELONA inajiandaa kuanzisha mazungumzo mapya juu ya mkataba na winga huyo wa Ufaransa, Ousmane Dembele. Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, unamalizika katikati ya mwaka 2022. ***(Mundo Deportivo)***

**WIJNALDUM AGOMBEWA**

BARCELONA na Bayern Munich zinajaribu kuwania saini ya mlinzi wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum, mwenye umri wa miaka 30, ambaye mwisho wa mwezi huu atakuwa mchezaji huru.***(Sky Sports)***

**HAZARD KURUDI CHELSEA**

NYOTA wa Real Madrid, Eden Hazard, mwenye umri wa miaka 30, anataka kurejea tena Chelsea, ambako aliondoka na kutua Santiago Barnabeu mwaka 2019. ***(El Chiringuito)***

**SOLSKJAER AMTAKA SANCHO**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameweka kipaumbele katika kumsajili Jadon Sancho mwenye miaka 21 baada ya msimu huu kukamilika, licha ya baadhi ya wachezaji kuishawishi klabu hiyo kumsajili kiungo wa Aston Villa na England, Jack Grealish mwenye miaka 25. ***(Telegraph)***

**NTCHAM ATAKIWA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle imefufua nia yao ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Celtic, Olivier Ntcham mwenye umri wa miaka 25. Mchezaji huyo yupo kwa mkopo Marseille. ***(Football Insider)***

## KMKM YATABIRIWA UBINGWA ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VITA ya kuusaka ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar imezidi kupamba moto huku mashabiki wakiitabiri timu ya KMKM kutwaa taji hilo msimu huu.

KMKM ambayo ndio kinara wa ligi hiyo, ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na alama 37 ikufutiwa na timu ya Mafunzo yenye alama 32 sawa na KVZ inayoshika nafasi ya tatu kutokana na kuzidiwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufunfwa wakati huu timu zote 12 zinazoshiriki ligi hiyo zikiwa zimebakisha mechi tatu kabla ya msimu kumalizika.

Kwa upande wa timu zinazoshuka daraja bado hazijajulikana kutokana na timu tano kutoka mkiani zote kupishana kwa alama ndogo katika msimo wa ligi licha ya mabingwa wa tetezi, Mlandege kuburuza mkia pamoja na Hard Rock ambayo nayo ipo katika mstari wa hatari wa kushuka.

Timu ya Kipanga nayo hapo jana baada ya kupoteza mchezo wake dhidi ya Malindi kwa kufungwa mabao 2-0 imeingia katika horodha ya timu ambazo zikifanya vibaya mechi zake zilizobaki kuna uwezekano wa kushuka msimu huu.

## RC IRINGA ATOA NENO LIPULI FC

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

WAKATI timu ya Lipuli FC ikitarajia kujua hatma yake Jumamosi ya safari ya kubaki Ligi Daraja la Kwanza ama kushuka itakapocheza mechi ya mchujo (Play Off) dhidi ya Fountain Gate FC, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amewataka wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi kwenda kuishangilia.

Baada ya mchezo wa awali kutoka sare ya bao 1-1, timu hizo Jumamosi zitashuka katika Uwanja wa Gairo, Dodoma kucheza mechi hiyo na mshindi wa jumla atabaki Ligi Daraja la Kwanza huku itakayopoteza itacheza tena mchezo wa mchujo dhidi ya timu ya Daraja la Pili kujua hatima yake ya kubaki ama kushuka.

Sendiga alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa shughuli ya makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, ambaye kwa sasa ni mkuu wa mkoa wa Tabora.

"Jamani Jumamosi ya Mei 29, timu yetu ya 'Wanapaluhengo' Lipuli FC inacheza 'play off' na Fountain Gate FC, tujitokeze kwa wingi kuipa nguvu kwani inabeba jina la Mkoa wa Iringa, kama kunatofauti tuziache tuinusuru hii timu isizidi kushuka," alisema Sendiga.

# SIMBA, AZAM KUTAFUTANA ROBO FAINALI FA CUP LEO

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Kombe la Shirikisho la Azam FC (ASFC), Simba, leo watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwenye mechi ya robo fainali ya michuano hiyo dhidi ya Dodoma Jiji FC, huku wakiwa na malengo ya kuendeleza ubabe wao baada ya kutoka kifua mbele mara zote tatu timu hizo zilipokutana Ligi Kuu. Hata hivyo, mapema kabla ya Simba kushuka dimbani dhidi ya Dodoma Jiji saa 1:00 usiku leo, majira saa 10:00 alasiri kutakuwa na mtanange mwigine wa hatua ya robo fainali kati ya wenyeji Rhino Rangers na Azam FC kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga na washindi wa michezo hiyo miwili watakutana nusu fainali.

**Kikosi cha Simba kinachonolewa na Kocha Mfaransa Didier Gomes, ambaye amedhamiria kufanya vizuri katika michuano hiyo na ile ya Ligi Kuu, amesema anaamini wanaweza kutekeleza malengo hayo kwa kuwa ana kikosi bora.**

"Haitakuwa mechi rahisi kwetu dhidi ya Dodoma Jiji, tuliweza kuwafunga kwenye mechi mbili za ligi, lakini haimaanishi hii itakuwa nyepesi, kwenye mashindano kadri yanavyozidi kupiga hatua yanakuwa magumu," alisema.

Lakini kwa upande wa Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema nyota wote wa kikosi chao wameendelea vizuri na maandalizi yao kama kawaida kuelekea mchezo wao huo wa ASFC.

Kuhusu hali ya nyota wawili, Thadeo Lwanga na Joash Onyango, waliuomia katika mchezo uliopita wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs, baada ya kugongana katika harakati za kuokoa hatari, alisema wote wanaendelea vizuri.

Kwa upande wa Azam FC, itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kutolewa kwenye michuano hiyo msimu uliopita hatua kama hiyo dhidi ya Simba ilipochapwa mabao 2-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Julai Mosi mwaka jana.

Rhino inatumia Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga badala ya Ali Hassan mwinyi, Tabora kutokana na uwanja huo kuwa kwenye ukarabati kwa ajili ya kuchezwa hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati amesema kuwa wataingia kwa tahadhari kwenye mechi hiyo kutokana na kutoifahamu vema Rhino Rangers.

"Tutaingia kwa tahadhari kwa sababu hatuifahamu vema timu hiyo ikoje, ina nguvu gani na inacheza vipi, hivyo inabidi tuwe makini kwa sababu wao watakuwa wanatufahamu sana kwa sababu wanatuona kila wiki tunacheza Ligi Kuu," alisema kocha huyo.




Kocha wa timu ya mpira wa miguu ya vijana na watoto ya TanZebras FC, Martin Hammel (kushoto), kutoka Ujerumani akimvalisha medali ya fedha mmoja wa wachezaji wa timu hiyo, Kelvin Mazika, kwa ushirikiano bora wakati wa hafla ya kuwaweka pamoja wazazi na watoto iliyoandaliwa na timu hiyo jijini Dar es Salaam juzi. Timu hiyo ni muunganiko wa timu ya Tanzania na Ujerumani. PICHA: JUMANNE JUMA

# Somoe akosa mpinzani uchaguzi TAWFA

**Na Saada Akida**

WAGOMBEA wawili katika nafasi ya Katibu Mkuu na Msaidizi, Someo Ng'itu na Veronica William, wamekosa wapinzani kuelekea uchanguzi mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TAWFA), ambao unatarajiwa kufanyika Juni 26, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi wa TAWFA, George Mushumba, ameliambia gazeti hili kwamba kikao cha Mei 23, kimewapitisha Somoe na Veronica katika mchujo wa majina ya wagombea nafasi mbalimbali.

Aliwataja wagombea ambao hawakuwa na mpinzani kuwa ni nafasi ya Katibu Mkuu, Somoe, ambaye anaomba ridhaa kwa mara nyingi baada ya muda wake kumalizika na Veronica anayegombea nafasi hiyo ya usaidizi.

Mwingine aliyekosa mpinzani ni nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Zena Chande.

Nafasi ya Mwenyekiti wako wawili ambao ni Amina Karuma na Sarah Chao wakati Makamu Mwenyekiti wanaogombea ni Roseleen Kusiwa na Beatrice Mgaya.

Katika nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendani ya TWFA, waliopitishwa kugombea ni nane ambao ni Suzana Ernest, Ndinagwe Richard, Lucas Peter, Mwanaisha Balisa, Emma John, Irine Deodatus, Jackline Jones na Mwanakheri Khatibu.

"Usaili wa wagombea utafanyika Mei 29 kuanzia saa tatu asubuhi katika Ofisi za TFF, Makao Makuu Karume-Dar es Salaam.


"Pingamizi dhidi ya mgombe au wagombea liwasilishwe kwenye Kamati ya Uchaguzi ya TAWFA mnamo au kabla ya Mei 27, mwaka huu saa kumi jioni," alisema Mushumba.

Alisema endapo kutakuwa na pingamizi au mapingamizi, yatasikiliswa Mei 28, mwaka huu kuanzia saa sita mchana.

# Michezo

Jumatano Mei 26, 2021

Nipashe

BENZEMA: SIONI ZIDANE AKIONDOKA REAL MADRID

HABARI UK 22

MABILIONI...




Rais wa TFF, Wallace Karia (Kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. bilioni 225.6 kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Azam Media, Tido Mhando, jijini Dar es Salaam jana baada ya kuingia mkataba mpya wa miaka 10 wa kuendelea kurusha matangazo ya Ligi Kuu Tanzania Bara utakaoanza msimu wa 2021/22 hadi 2030/31. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YANGA YAIFUATA BIASHARA NUSU FAINALI KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na winga Deus Kaseke, jana yameipeleka Yanga kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA kwa kuiadhibu Mwadui FC 2-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

Yalikuwa ni makosa ya kizembe ya kipa Mussa Mbissa, yaliyoizawadia Yanga bao dakika ya 25, alipotaka kuleta mbwembwe za kumpiga chenga Kaseke, lakini mchezaji huyo aliunasa mpira na kuujaza wavuni.

Kipa huyo alikuwa amerudishiwa mpira na beki wake, Khalfan Mbarouk, pembeni mwa uwanja na haukuwa na madhara yoyote, lakini alichofanya ni kurudi nao ndani ya 18 na kumsubiri Kaseke ampige chenga, badala yake akaigharimu timu yake bao hilo baada ya kupokonywa mpira na winga huyo.

Kaseke tena, aliwainua vitini wanachama, mashabiki na wapenzi wa timu hiyo, alipoukimbilia mpira mrefu uliopigwa na Yacouba Sogne na kuwazidi mbio mabeki wa Mwadui, kabla ya kuujaza wavuni dakika ya 56.

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilitawala hasa katikati mwa uwanja, lakini ilishindwa kutumia nafasi nyingi zilizopatikana kufunga mabao kutoka kwa Feisal Salum aliyekosa mabao mawili ya wazi, Yacouba aliyeshindwa kukwamishwa wavuni akiwa na kipa Mbissa mara tatu. Nafasi pekee ambayo ilipatikana kwa Mwadui, ilikuwa ni dakika ya 39, baada ya Jabir Aziz kuikosesha timu yake bao, alipopiga shuti juu ya lango la Yanga akiwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga. Kwa matokeo hayo, Yanga sasa itapambana dhidi ya Biashara United kwenye mechi ya nusu fainali.

# BILIONI 225 ZAMWAGWA LIGI KUU BARA

## ●●●Nne bora ni vita ya kuchafuka noti, itakayoburuza mkia nayo kulamba mamilioni huku bingwa akiondoka na...

**Na Saada Akida**

MBIO za kuwania kumaliza nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, zimeongezewa thamani kwa kipindi cha miaka 10, kuanzia msimu ujao wa 2021/22 hadi 2030/31, ambapo sasa timu zitakazomaliza nne-bora zitaondoka na mamilioni ya shilingi, huku pia itakayoburuza mkia ikiondoka na kitita cha maana, imeelezwa.

Hatua hiyo, imekuja baada ya jana Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kusaini mkataba mnono wa miaka 10 wenyewe thamani Sh. bilioni 225.6 na Azam Media Limited wa kuendelea kurusha matangazo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia msimu wa 2021/22 hadi 2030/31.

Uboreshwaji wa zawadi hizo kwa Ligi Kuu Bara, hautaiacha klabu yoyote shiriki kutoka patupu mfumo ambao umekuwa ukitumiwa na Ligi Kuu England ambayo mlolongo wa zawadi huanzia juu hadi kwa timu inayoburuza mkia.

Kwa bingwa wa Ligi Kuu Bara, kuanzia msimu ujao atapata bonasi ya Sh. milioni 500 kutoka kwa wadhamini hao, mshindi wa pili Sh. milioni 250, wa watatu milioni 225 na msindi wa nne ataibuka na Sh. milioni 200, nafasi ya tano milioni 65, ya sita milioni 60, ya saba milioni 55, ya nane 50 na ya tisa milioni 45.

Timu itakayoshika nafasi ya 10 itaondoka na milioni 40, ya 11 milioni 35, ya 12 milioni 30 ya 13 milioni 25 na itakayoangukia kucheza mechi ya mchujo 'Play off', italamba milioni 25. Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema kiwango hicho cha fedha zitagawiwa klabu za ligi hiyo na watatakiwa kuzitumia katika mambo ya msingi ikiwamo kulipa mishahara, bima za afya pamoja na usafiri wa timu.

Alisema katika gawio la fedha hizo, hazitakuwa sehemu ya fungu la usajili wa wachezaji au kulipa madeni klabu wanayodaiwa na wachezaji na makocha ambao walioachwa awali bila kulipwa.

"Tutatoa fedha hizi katika klabu ambazo zitaleta mchanganuo wake, lakini zitazokabidhi ripoti ya mapato na matumizi kwa mwaka, klabu isipofanya hivyo haitapata fedha hizo na watakaopata zitaingizwa katika system (mfumo)," alisema Karia.

Alisema Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) itatoa semina kwa viongozi wa fedha wa klabu hizo kwa lengo la kuhakikisha zinatumika kwa weledi na kuwapo kwa uadilifu.

Naye Mtendaji Mkuu wa Azam Media, Tido Mhando, alisema hawana shaka kwa kiasi hicho cha uwekezaji kwani kinatoa nafasi kwa klabu kujiimarisha na kuongeza ushindani mkubwa.

"Huu ni mwaka wa nane tangu Azam Media kuwa na haki ya kuonyesha matangazo ya Ligi Kuu na tunaendelea kuonyesha mpira wetu, hivyo ni nafasi kubwa kwa wachezaji kujiuza na kufanya kazi vizuri," alisema Mhando.

Alisema mgawanyo wa fedha hizo uzingatiwe na thamani ya soka na kugawana na klabu kwa asilimia 68 ya fedha za malipo ya kila msimu katika mkataba huo na zinaenda moja kwa moja kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu.

"Fedha hizo zitakuwa zikiongezeka kila msimu na ndio maana utaona msimu wa 2022/23 fedha zitakazotolewa ni Sh. bilioni 13.2 huku timu zikipata Sh. bilioni 8.8, msimu wa 2030/31 zitatolewa Sh. bilioni 28 huku klabu zikichukuwa Sh. bilioni 19," alisema.

Mhando alisema katika fedha hizo kutakuwa na bonasi kwa miaka mitatu ya msimu ujao kwa bingwa wa Ligi Kuu kulamba Sh. milioni 500, mshindi wa pili Sh. milioni 250, wa watatu Sh. milioni 225 na msindi wa nne ataibuka na Sh. milioni 200.

Alisema bonasi hiyo itatolewa kwa klabu zote ikiwamo klabu inayoshiriki pamoja na timu itakayocheza 'Play off' ya kubaki Ligi Kuu nayo itapata Sh. milioni 20.

Kwa upande wa wakilishi wa klabu, Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema mkataba huo una manufaa kwa klabu zao kufanya vizuri na kuzisaidia timu ambazo hazina wadhamini.

"Kiasi cha fedha hizi zitaweza kutusaidia katika shughuli zetu za timu, ikiwamo kusafiri, sehemu ya malazi maana kuna klabu zingine hupata changamoto, nina imani kwa udhamini huu tuwapongeze TFF na Azam Media kushinda zabuni hiyo," alisema Barbara.

Naye mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amini 'Popat', alisema: "Udhamini huu utaleta ushindani mkubwa kwa klabu kupambana na kufanya vizuri.

"Timu zitaweza kujiendesha vizuri na nina imani kila klabu itahitaji kupambana kuhakikisha inafanikiwa kupata fedha ukizingatia kila mshiriki anapata fedha kwa viwango tofauti, kwa bingwa kupokea Sh. milioni 500 na anayemaliza nafasi ya 13 anapokea Sh. milioni 25," alisema Popat.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002